MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

## ‘Shahidi alimtambua mtuhumiwa kwa kumshika bega’



UKURASA 4

## Wapigambizi wagundua sauti za kutisha wakitafuta nyambizi ya Titan

UKURASA 19



ama

ALHAMISI JUNI 22, 2023

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

DC Jokate abuni mbio za wajawazito zenye washiriki 2000, zilivyotia fora

Waziri Makamba: Hii hapa mikakati rasmi kupata umeme wa jotoardhi

Ukurasa 14

Vita Mazingira vya Rais, mchanganuo wake unavyojitokeza kwenye bajeti

•Dola milioni 33.9 mezani ya miradi mikakati

Na Jenifer Gilla, aliyekuwa Dodoma

TANZANIA kama zilivyo nchi nyingine inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri uchumi wake, ikiwamo kwenye uzalishaji wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na utalii.

Ni alhamisi ya wiki iliyopita, bungeni kuliwasilishwa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali, ambayo sasa yanaendelea kujadiliwa, ikibeba msimamo na mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhusu anachonuia kuwatekelezea wananchi kitaifa, kwa huduma na maendeleo.

Akibeba wajibu wa rais bungeni, Dk. Mwigulu anawakumbusha mawaziri husika wa sekta za mazingira na mabadiliko ya tabianchi, waandae miradi sahihi, ili wanufaike na fedha hizo.

Anafafanua: "serikali inaendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo ili kuongeza fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi."

Dk. Mwigulu anapendekeza kutozwa ushuru wa bidhaa kwa asilimia 10 kwenye magari ya abiria yanayoingizwa nchini yanayozidi umri wa miaka mitano (magari chakavu), huku kukifutwa ushuru wa forodha kwa mabasi ya abiria kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Vilevile anapendekeza kutozwa ushuru wa bidhaa za magari asilimia tano, kwenye magari yenye uwezo wa injini kati ya lita za ujazo 1000 hadi 2000 na kutoza ushuru asilimia 10 kwenye magari yenye uwezo lita za ujazo 2000.

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Juni 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581349

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Tozo miamala simu kufutwa

• **Muswada** watua rasmi bungeni, Kodi ya Majengo kuongezwa... *Endelea ukurasa 2*



## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WABUNGE WALIA NA ONGEZEKO SH. 100/- KILA LITA YA MAFUTA

WABUNGE wameitaka serikali kutafakari upya mapendekezo ya kuongeza Sh. 100 kwenye kila lita ya mafuta ya dizeli na...

UKURASA WA 4

### PM ATAKA VIONGOZI DINI KUKEMEA HADHARANI MMOMONYOKO MAADILI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini nchini kutojiweka kando katika...



## Ajali ya lori na basi ilivyyoua 7, kujeruhi 49 Njombe

UKURASA 2



## Lipumba aichambua bajeti, atoa angalizo

UKURASA 3

**MICHEZO** **MSUVA AIPA YANGA NAFASI KUMSAJILI** UK.24

**KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Ajali ilivyoua watu saba, kujeruhi 48

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU saba wamefariki dunia huku 49 wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi la kampuni ya New Force lenye usajili namba T 173 DZU lililoingia mtaroni katika Kijiji cha Igando, Kata ya Luguda wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, John Imori, aliwaambia waandishi wa habari eneo la tukio kuwa ajali hiyo ilitokea Juni 21 saa nane na nusu mchana wakati basi hilo linalofanya safari zake za Dar es Salaam-Rukwa lilipokuwa linalipita lori.

"Chanzo cha ajali ni hili basi la abiria la New Force lilikuwa linatokea jijini Dar es Salaam kwenda Sumbawanga (Rukwa) lilipofika hapa Igando kuna sehemu ya daraja likawa linataka kulipita lori, likapoteza mwelekeo, likagonga daraja, likaingia mtaroni," alisema Imori.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Lutheran Ilembula, Dk. Pangamawe Kidenya, alisema walianza kupokea miili ya marehemu na majeruhi saa 10 jioni.

"Tulipokea maiti tano majira ya saa 10 jioni lakini wakati tunaendelea na huduma, imeongezeka moja, hali zao wanaendelea vizuri lakini wengine wawili wamepoteza fahamu," alisema Dk. Kidenya.

Baadaye Kamanda Imori aliwaambia waandishi wa habari kuwa hadi kufikia saa 1:10 usiku, walibaini kuwapo mwili wa mtu uliokuwa umenasa kwenye basi, wakati huo rekodi ya vifo kutokana na ajali hiyo ilikuwa saba.

# Tozo miamala simu kuondolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023, umependekeza marekebisho kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306 kwa kufuta kifungu cha 164A, ili kufuta tozo ya muda wa maongezi kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji.

Aidha, kufutwa tozo ya miamala ya kuhamisha fedha kielektroniki ili kuondoa uwezekano wa kiwango cha fedha kutozwa mara mbili na kuchochea ufanyaji wa malipo ya kielektroniki.

Septemba 30, 2022, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kupitia gazeti la serikali alitangaza mabadiliko kupitia Sheria ya Mifumo ya Malipo (Sura ya 437) chini ya kifungu cha 46A (2), ambazo zilianza kutumika Oktoba mosi, mwaka jana.

Aidha, jedwali la marekebisho hayo, kuhamisha Sh. 100 hadi 2,999 ni Sh. 10, kuhamisha Sh. 3,000 hadi 3,999 ni Sh. 14, Sh. 4,000 hadi 4,999 ni Sh. 27, kutuma Sh. 5,000 hadi 6,999 ni Sh. 54, kutuma 7,000 hadi 9,999 ni Sh.56.

Vingine ni kutuma Sh. 10,000 hadi 14,999 ni 102, kutuma Sh. 15,000 hadi 19,999 ni Sh.195, kutuma Sh. 20,000 hadi 29,999 ni Sh.306, kutuma Sh. 30,000 hadi 39,999 ni Sh. 351, kutuma Sh. 40,000 hadi 49,999 ni Sh. 419, kutuma Sh. 50,000 hadi Sh. 99,999 ni Sh. 573, kutuma Sh.100,000 hadi 199,999 ni Sh. 707, kutuma Sh. 200,000 hadi 299,999 ni Sh.821.

Kutuma Sh.300,000 hadi 399,999 ni Sh.838, kutuma 400,000 hadi 499,999 ni Sh.982, kutuma 500,000 hadi 599,999 ni Sh1,245, kutuma 600,000 hadi 699,999 ni Sh1,532.

Kutoka 700,000 hadi 799,999 ni Sh.1,700, kutuma 800,000 hadi 899,999 ni Sh.1,500, kutuma 900,000 hadi 1,000,000 ni Sh.1,776, kutuma 1,000,001 hadi 3,000,000 ni Sh.1,875, kutuma 3,000,001 na kuendelea 2,000.

### KODI YA MAJENGO

Vile vile, unapendekeza kuongezwa kwa kodi ya majengo kwa mwaka, majengo ya ghorofa na yasiyo ya ghorofa huku nyumba za tope, fito, tembe, nyasi na zinazofanana na hizo kwa ajili ya makazi kutohusishwa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Mwigulu Nchemba, alitoa mapendekezo hayo jana bungeni alipokuwa akiwasilisha muswada huo wenye mapendekezo mbalimbali ya marekebisho ya mifumo ya kikodi.

Viwango vya kodi vinavyopendekezwa kwa majengo hayo ni kutoka Sh. 12,000 hadi Sh.18,000 kwa yasiyo ya ghorofa na kutoka Sh. 60,000 kwenda Sh. 90,000 kwa kila sakafu ya ghorofa ili kodi iakisi thamani halisi ya majengo hayo.

Alisema muswada huo unapendekeza marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289 kwa kurekebisha kifungu cha sita ili kujumuisha maeneo yote ya wilaya katika utozaji wa kodi ya majengo isipokuwa majengo yaliyosamehewa katika sheria ili kuweka usawa kwenye ulipaji kodi.

Pia, muswada huo unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 kwa kuongeza kifungu kipya cha 33A, ili kuwezesha halmashauri kukasimiwa jukumu la kukusanya kodi ya pango la ardhi kwa niaba ya wizara yenye dhamana na masuala ya ardhi na kurejeshewa asilimia 20 ya mapato yatakayotokana na kodi ya ardhi kuziwezesha halmashauri katika usimamizi, ukusanyaji na ufuatiliaji wa kodi hiyo.



### TOZO CD, DVD MEMORI KADI

Muswada huo unapendekeza pia marekebisho katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa kurekebisha kifungu cha 48A ili kutoza tozo ya asilimia 1.5 kwenye vinyl, mini disc, compact disk (CD), digital versatile disk (DVD) na SD memory ili kuimarisha usimamizi wa hakimiliki katika kazi za ubunifu.

### USHURU WA BIDHAA

Alisema muswada unapendekeza kurekebishwa kwa kubadili utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kutoka kila mwaka na kuwa kila baada ya miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema lengo la marekebisho hayo ni kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji.

Kadhalika, alisema vifungu 124(5A) na (5B) vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari ya abiria yanayotumia teknolojia ya kisasa (hybrid vehicles) yaliyotumika kwa zaidi ya miaka mitano tangu yalipotengenezwa ili kupunguza uingizaji wa magari chakavu na kulinda usalama wa abiria.

### MAKADIRIO YA KODI

Alisema muswada unapendekeza kurekebisha utaratibu wa ukadiriaji kodi ya mapato kwa walipa kodi binafsi ambao wanafanyabiashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo na hawana wajibu wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi.

"Kifungu cha 56 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa miamala ya utoaji wa hisa mpya na uhamishaji milki ya kampuni unaofanywa na wanahisa wakazi katika utozaji wa kodi ya mapato ili kuvutia uwekezaji nchini," alisema.

Kadhalika unapendekeza kufuta na kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari kwa walipakodi binafsi ambao hawana wajibu kisheria kuwasilisha ritani za kodi.

### KODI YA ZUIO

Alipendekeza kuondoa wajibu kwa watu binafsi kukata kodi ya zuio kwenye upangishaji wa nyumba, ili kuondoa wajibu kwa wapangaji wasiofanya biashara kulipa kodi ya zuio kwa niaba ya wenye nyumba.

Muswada unapendekeza marekebisho ili kuweka kiwango cha kodi ya asilimia tatu ya thamani ya mauzo au thamani ya ardhi kwa wauza ardhi wasiokuwa na uthibitisho wa nyaraka zinazoonesha gharama alizotumia, ili kuweka utaratibu rahisi wa ukokotoaji wa kodi ya ongezeko la mtaji kwa mauzo ya ardhi kwa wauzaji ambao hawana nyaraka.

### TOZO UFUNDI STADI

Dk. Mwigulu (pichani), akiwasilisha muswada huo, alisema unapendekeza kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi stadi kutoka asilimia nne hadi 3.5 ili kuwapunguzia waajiri gharama za uendeshaji wa shughuli zao.

# Wabunge walia Sh.100 ongezeko kodi ya mafuta

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kutafakari upya mapendekezo ya kuongeza Sh. 100 kwenye kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli, kurahisisha utoaji risiti kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Wakichangia jana mjadala wa mapendekezo Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24, walisema iwapo kutakuwa na ongezeko hilo itakuwa ni mzigo kwa wananchi wa hali ya chini.

Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, alishauri serikali kuangalia namna nyingine ya kukusanya kodi badala ya kuongeza Sh. 100 kwenye mafuta ya dizeli na petroli kwa kuwa kufanya hivyo kutawaongezea mzigo wananchi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo, alishauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuboresha mifumo ya utoaji risiti za malipo kwa maofisa wao ili wawe na uwezo wa kutoa mahali popote na kurahisisha huduma ya kulipa madeni na ukusanyaji wa kodi.

Pia alipendekeza serikali iangalie namna nyingine ya kukusanya mapato hasa kipindi ambacho Dola ya Kimarekani inazidi kupanda kudhibiti kwa bidhaa na huduma ikiwamo daladala, mabasi na vyakula.

Alisema kwenye mafuta pekee kuna kodi zaidi ya 22, ikiwamo Sh. 413 ikijumuisha Sh.186 kwa ajili ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Sh. 177 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Sh. 50 kwa ajili ya maji, ambazo zinahusika na barabara.

Kuhusu ongezeko la Sh. 20 kwa kila kilo moja ya saruji, alisema kutaongeza gharama za ujenzi na kurudisha nyuma lengo la serikali la kuondoa nyumba za udongo kwa kuwa Watanzania hawataweza kumudu gharama hizo.

### BANDO LA SIMU

Gambo aliishauri serikali kuangalia upya gharama za mabando ya simu, kwa kuwa zimekuwa moja ya tozo zinazowaumiza wananchi.

Alisema mwaka 2020 bando mtandao wa Vodacom la GB 10 lilikuwa linauzwa Sh. 15,000, lakini leo kiasi hicho cha fedha unapata bando la GB 7.38 huku Tigo na Airtel ukipata GB 7.2.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya (CCM), Suma Fyandomo, alishauri serikali kuboresha mfumo wa kutoa risiti za kulipia madeni ili maofisa waweze kutoa wakiwa katika operesheni ya kukamata vyombo vya moto kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi.

Alisema hali hiyo inarudisha nyuma utendaji kazi wa wafanyabiashara hao kwa sababu wanapokamatwa na kutakiwa kulipa deni inawalazimu kwenda kwenye ofisi za TRA na kuwapotezea muda wao.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega, aliitaka serikali kuwapunguzia mzigo wa kodi wananchi kwa kuweka mazingira rahisi kwa vijana na makundi mengine kupata mikopo ya bei nafuu na kuwawezesha kiuchumi, ili kuongeza vyanzo vya kukusanya mapato.

Pia aliiomba serikali kuweka kodi inayolipika ikiwamo ya magari ili wananchi wengi wajiajiri na kutengeneza ajira kwa wengine kinyume cha hayo inatengeneza mianya ya rushwa kwa wafanyabiashara kukubali kutokulipa kodi.

# Lipumba aichambua bajeti, aja na angalizo

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, ameyachambua mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24, na kushauri mengi yaliyomo yalipaswa kuwa kwenye bajeti za wizara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mapendekezo hayo yenye kurasa 227 yaliyowasilishwa bungeni Alhamisi iliyopita, baadhi ya mambo hayasaidii kuelewa utekelezaji wa bajeti ya 2022/23 na malengo ya bajeti ya 2023/24.

"Mambo muhimu ya kibajeti kama vile utekelezaji wa bajeti ya 2022/23 yameelezwa kwenye kurasa tano tu (56 - 60)," alisema.

"Hotuba ya bajeti haiendelezi 4R za Rais...imewasilishwa kama vile ni ya wana CCM badala ya kulenga kuwaunganisha Watanzania wote," alisema.

Alisema Wizara ya Fedha na Mipango inapaswa kuchambua kwa kina ukuaji wa uchumi kutoongezeka kwa kasi kubwa baada ya kupungua janga la UVIKO-19.

Pia, hotuba ya bajeti na hali ya uchumi haionyeshi dira ya kukuza uchumi kwa asilimia nane hadi asilimia 10, ili wafanikishe kuongeza ajira na kutokomeza umaskini.

Kwa mujibu wa Lipumba, makadirio hayo yamerudia takwimu za umasikini za kiwango cha asilimia 26.2 cha mwaka 2017/18 na kigezo cha kitaifa cha nani masikini anayetumia chini Sh. 49,320 kwa mwezi.

Alisema hotuba hiyo haichangambua kwa kina hali ya uchumi na kuyatafutia majibu.

"Ni vyema uchambuzi wa kina wa mafanikio ya Mfuko wa Maendeleo wa Kaya Maskini (TASAF) ufanywe kwa lengo la kuakisi sera ya kupambana dhidi ya umaskini kwa kutekeleza sera ya kipato cha msingi kwa wote tukianza na wazee, wajawazito na wenye watoto wachanga," alisema.

Aidha, Prof. Lipumba alishauri kufanywe utafiti wa kina wa namna Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inavyokadiria mfumko wa bei na kufanya marekebisho ili pawe na uhalisia wa makadirio ya mfumko wa bei.

"Tunarudia tena kushauri kufanya utafiti wa kina wa namna NBS linavyokadiria mfumko wa bei na kufanya marekebisho, ili pawe na uhalisia wa makadirio ya mfumko wa bei," alisema.

Alisema Waziri hakujadili changamoto za urari wa malipo ya nje zinazolikabili taifa na hajafanya uchambuzi wa mkakati wa kuongeza mauzo ya bidhaa za nje.

Kabla Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuingia katika biashara ya kununua dhahabu, alipendekeza kufanywe tathmini ya kina ya uzoefu wa miaka 80 wakati wakifanya hivyo, ili kujua sababu zilizofanya benki isiendelee na utaratibu huo kabla ya kuanza tena.

Kadhalika, uhimilivu wa deni la nje hivi sasa ni matokeo ya kusamehewa madeni mwaka 2000 na mwaka 2006.

"Waziri hakueleza hivi sasa tunalipa kiasi gani cha riba kwenye madeni ya kibiashara na tunatarajia riba hiyo kupungua kwa kiasi gani baada ya kufanyiwa tathmini ya uwezo wa Tanzania kukopa na kulipa madeni katika masoko ya kimataifa (Credit Rating)," alisema.

Changamoto zinazowakabili Watanzania kushiriki katika uchumi wa kidijitali, alisema hazikuainishwa na kutafutiwa ufumbuzi ndani ya bajeti hiyo.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo ambaye kitaaluma ni mchumi, alisema hotuba ya bajeti haina viashiria vya utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi cha rais cha ujenzi wa demokrasia upatikanaji wa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.



"Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura unapaswa kufanywa mara mbili kabla ya uchaguzi ujao. Hilo halimo katika hotuba ya bajeti," alisema.

Alisema hotuba ya Bajeti ya Mwaka jana ilieleza "kila mtanzania mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 na mwenye kipato anatakiwa kulipa kodi lakini hotuba ya bajeti ya mwaka huu, haitathimini utekelezaji wa sera na kama serikali inaendelea nayo au imeiacha.

Bajeti ya 2023/24 inatarajia kuwa na ziada ya Sh. trilioni 1.07 na kugharamia asilimia 7.6 ya bajeti ya maendeleo na kusema kwamba, ni vyema pakawa na hatua za makusudi kuendeleza kugharamia sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo kwa kutumia ziada ya bajeti ya kawaida.

### WABUNGE

Wakichangia mjadala wa mapendekezo ya bajeti bungeni, wabunge wametaka serikali kuja na mkakati wa kushusha bei ya nafaka kwa kuiagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua mazao hayo.

Mbunge wa Jimbo la Lupembe (CCM), Edwin Swalle, aliitaka serikali iiangize NFRA kununua mahindi ambayo yameanza kushuka bei kiasi cha wengi kukosa soko.

Vilevile, alimtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kufuatilia kwa karibu suala la utoaji wa vibali na leseni kwa wafanyabiashara wanaouza mazao nje ya nchi kwa kuwa wamekuwa wakisumbuliwa.

Akitoa taarifa, Waziri Bashe alisema NFRA imeshaanza kununua mahindi kwa bei ya chini ya Sh. 600 hadi 700 na Wameshafungua vituo na hivi karibuni watatoa taarifa vimefunguliwa wapi.

Aidha amesema serikali itaanza kutoa leseni kwa njia ya kielektroniki kuanzia Julai, mwaka huu ili kuwaondolea adha wafanyabiashara ya ucheleshwaji wa vibali hivyo kwa njia ya kawaida.

***Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Jenifer Gilla (DODOMA)***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

KESI YA MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

# ‘Shahidi alimtambua mtuhumiwa wa mauaji kwa kumshika bega’

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkaguzi wa Polisi, Modest Mallya (60), ameieleza mahakama kuwa mke wa marehemu, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita anayetuhumiwa kumuua wifi yake Aneth wakati anafanyiwa gwaride la utambulisho, hakuwa na pingu mkononi.

Aidha, amedai kuwa katika gwaride la utambulisho dada wa kazi wa marehemu Aneth, Getruda Mfuru, alimtambua kwa kumshika bega Miriam kuwa ndiye aliyehusika katika tukio hilo akiwa kwenye mstari wa washiriki wanane.

Mallya alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi dhidi ya Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wanaotuhumiwa kumuua Aneth, Mei 25, 2016.

Akijibu swali la wakili wa utetezi, Peter Kibatala, Mallya alidai kuwa kabla ya kufanya gwaride la utambulisho alijiridhisha kuwa mtuhumiwa Miriam hakuwa na pingu mkononi ndiyo maana hakuwa na pingamizi lolote kwenye zoezi hilo.

Pia, alidai kuwa Miriam katika gwaride hilo hakutaka kuwa na ndugu, jamaa, rafiki au wakili wa kushuhudia tukio hilo, kwa sababu alimweleza haki zake za msingi kuwa anaweza kuwa na watu hao, lakini yeye alikubali kuendelea na zoezi hilo bila hao kuwapo.

Akiendelea kujibu maswali ya Kibatala, Mallya alidai hajawahi kufutilia kama shahidi Mfuru aliwahi kuzungumza na msimamizi na mpelelezi wa kesi hiyo ASP David, kabla hajamtambua mtuhumiwa katika gwaride hilo.

“Wakati nafanya zoezi nilikuwa najua PGO 232 (h) inakataza mawasilisho kati ya mpelelezi wa kesi na shahidi mtambuzi, lengo la kukataza, wasipeane majibu, kabla ya utambuzi,” alidai Mallya.

Kabla ya maswali hayo ya Kibatala, Mallya akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, alidai Agosti 7, 2016 alikuwa Kituo cha Polisi Kilwa Road, akiwa na cheo cha Mkaguzi wa Polisi, alipata maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa (RCO) Mchovu, kuandaa gwaride hilo.

Alidai kuwa baada ya maandalizi yote ya gwaride ofisa polisi aliyeandaliwa kumleta mtuhumiwa kwake alipofika alijitambulisha na yeye alijitambulisha kwa jina la Miriam Steven na kumweleza haki zake za msingi.

“Katika majibu yote ya haki zake za msingi mtuhumiwa hakuleta pingamizi lolote kwangu alisema yupo tayari kushiriki gwaride la utambulisho na nilimweleza na zile haki za kuwa na ndugu, jamaa na marafiki yeye alisema atashiriki tu,” alidai.

Alidai kuwa Mrita alichagua kusimama mtu wa tano kutoka kushoto, hatua iliyofuata aliwaelekeza maofisa walioandaliwa wamlete shahidi, alijitambulisha kwake na yeye alitambulisha kwake kuwa ni Getruda Mfuru.

“Nilimfahamisha Mfuru jukumu ambalo alitakiwa kulifanya kuwa ni kupita kwenye mstari mbele na nyuma, ambapo alimtambua mtuhumiwa kwa kumshika bega Miriam Steven,” alidai.

Alida kuwa alimfahamisha ASP David kuwa tayari mtuhumiwa ameshatambuliwa na yeye anatakiwa kujaza fomu ya polisi namba 186, ambayo aliijaza majina yote ya washiriki na walisaini.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni aliyekuwa mke wa bilionea huyo, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela (40). Aneth aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, jijini Dar es Salaam.




Mkuu wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani wa Vodacom Tanzania PLC, Brigita Shirima (kushoto) na Meneja Mwandamizi wa Mauzo, Lwambano Kilumba (kulia), wakimkabidhi wakala wa usajili, Ally Buturo (katikati), zawadi ya jiko la gesi na mtungi wake baada ya kujikusanyia pointi nyingi kwa kusajili wateja wapya wengi na kununua salio na vifurushi kupitia M-Pesa kutokana na kampeni inayoendeshwa ya ‘Loyalty Program’ na kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM awataka viongozi dini kukemea hadharani mmomonyoko maadili

**Na Asraji Mvungi,** ARUMERU

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini nchini kutojiweka kando katika jukumu lao la kurekebisha mifumo ya maisha kwenye jamii na kurejesha maadili ya utu wa binadamu.

Aidha, amewaomba kujitokeza hadharani kukemea na kulaani, ongezeko la matukio ya ubakaji na ulawiti yanayolitesa taifa kwa sasa.

Majaliwa aliwapa kibarua hicho viongozi wa dini jana, alipokwenda katika Chuo cha Biblia Sakila, kilichoko Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, kushiriki maadhimisho ya miaka 40 ya kuzaliwa kwake.

“Viongozi wa dini, endeleeni kukemea vitendo viovu na vinavyotishia ustawi wa amani na maadili ya nchi yetu, ikiwamo ubakaji, ulawiti na mmomonyoko wa maadili hasa kwa vijana.

“Ni lazima dini zitumike ipasavyo kurekebisha mifumo ya maisha katika jamii na kurejesha maadili ya utu wa binadamu kama vinavyoelekeza vitabu vitakatifu vya dini ili kuhakikisha matokeo yanaonekana.”



Kuhusu malalamiko ya wananchi ya kutotekelezwa kwa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Sakila/Kikatiti, Waziri Mkuu, alisema ahadi hiyo iko pale pale.

Katika kutekeleza dhamira hiyo, Waziri Mkuu, ameagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kuanza maandalizi ya kutekelezwa kwa ahadi hiyo.

Kuhusu malalamiko ya vikwazo katika usajili wa taasisi za dini, Waziri Mkuu, alisema uamuzi wa kubana mianya katika eneo hilo, unalenga kuongeza ustawi wa taasisi hizo na kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Vilevile, alitoa ufafanuzi kuhusu malalamiko ya kodi za kuingiza mizigo na vifaa vya madhehebu ya dini, akisema lengo ni udhibiti wajanja wachache wanaotumia fursa hiyo kujinufaisha na kufanya biashara, suala ambalo haliwezi kukubalika.

Askofu Mkuu wa Kanisa la International Evangelism Centre Tanzania na Mkuu wa Chuo cha Biblia Sakila, Eliud Isangya, aliishukuru serikali kwa kujenga mazingira ya kuwaweka karibu viongozi wa dini, na wa kisiasa kwa kuwa jambo hilo linaongeza umoja na ushirikiano na wananchi.

## PSSSF yakabidhi vifaa tiba Wiki Utumishi wa Umma

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umekabidhi vifaa tiba kwa vituo vya afya, Mkunguni na Dimbani, Wilaya ya Kusini Unguja, Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

Tanzania huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kila Juni 23 ya mwaka ili kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika Maendeleo ya taifa lolote duniani.

Hapa nchini maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yameanza Juni 16 na yatafikia kilele Juni 23 na kwa mwaka huu yanabeba kaulimbiu; “Kufanikiwa kwa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (Acfta) Kunahitaji usimamizi wa Utumishi wa Umma Wenye Mtazamo wa Kikanda”.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo Mkurugenzi wa Fedha PSSSF, Beatrice Musa-Lupi ambaye alifuatana na Meneja wa PSSSF Zanzibar, Amina Kassim na Meneja Utawala, Gloria Mboya, alisema Mfuko umeamua kuadhimisha siku ya Utumishi wa Umma kwa kutoa msaada wa vifaa tiba kwa vituo hivyo vya afya kwa kuthamini mchango mkubwa wa watumishi wa umma katika kuleta maendeleo na ustawi katika jamii yetu.

“Vifaa tiba tulivyokabidhi leo vitawezesha utoaji huduma bora na za hali ya juu kwa wagonjwa wetu, tumetoa vifaa kama vile mashine za kupima, vifaa vya kuimarisha usafi, vifaa vya kusaidia uchunguzi wa magonjwa, viti mwendo na vipoza hewa (viyoyozi) ni imani yetu vifaa hivi vitatumika kwa ufanisi na kuleta mabadiliko chanya katika afya ya wananchi wetu,” alifafanua.

Alisema Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), ilitoa maelekezo ya namna nzuri ya Taasisi za Umma kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kukutana na watumishi wanaofanya kazi maeneo ya pembezoni ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo katika kuwahudumia wananchi.

Alisema Mfuko unatambua kuwa changamoto za kifedha na rasilimali zinaweza kuwapo, lakini hatua hiyo ya kujitolea na kushirikiana na taasisi zingine, inaweza kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya afya.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kusini Unguja, Omar Mohamed Kasongo aliushukuru Mfuko wa PSSSF kwa misaada hiyo na kusema huduma ni sehemu ya tiba, vifaa hivyo vitasaidia kuboresha tiba kwenye vituo hivyo vya afya na kuwanufaisha wananchi wa maeneo hayo.

## TANGAZO


The Guardian
www.ippmedia.com
The Home of Great Newspaper

# Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*

**ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS**

**HEAD OFFICE**

THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz
The Guardian @Theguardiantz
IPPmedia .com

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Wateule wa Rais tekelezeni wajibu wenu msimwangushe*

**MARA** kwa mara Rais Samia Suluhu Hassan anapofanya uteuzi wa viongozi katika taasisi mbalimbali, amekuwa akisisitiza uwajibikaji kwa kutekeleza majukumu yao bila upendeleo wowote ili kuondoa malalamiko kwa wanaopatiwa huduma hizo.

Hata hivyo, kuna baadhi wa watendaji wanapopewa nafasi hizo baada ya muda wanajisahau na jukumu walilopewa hawalitekelezi ipasavyo na kuzua malalamiko.

Hali hiyo humlazimu kila mara Rais kutengua na kuteua ili kuhakikisha kazi anayokusudia ifanyike kwa ufanisi inatekelezwa.

Kati ya watendaji waliopewa jukumu la kutumikia wananchi ni Kabidhi Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), ambaye baada ya kuingia ofisini aliwakumbusha watumishi kujipanga ili kuwafikia wananchi wanaohitaji huduma na kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara.

Wakati akiwaapisha wateule wake wiki iliyopita Rais Samia, alitaja sababu ya kuwatumbua waliokuwapo kwenye nafasi hiyo kuwa ni kutokutekelezwa kwa kazi vizuri na ugomvi.

Ni jambo la aibu kwa viongozi wanaotakiwa kufanyakazi kwa ushirikiano, wakianza kuonyesha mfano mbaya kwa walio chini yao kwa kugombana na kusababisha kazi kutotendeka kwa ufanisi.

Wakati akizungumza katika kikao cha wafanyakazi baada ya kuanza kazi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, aliwataka wafanye kazi kwa ushirikiano, umoja na upendo ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao na kuwawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi wanaowahudumia.

Aliwakumbusha kuwa RITA ni taasisi nyeti inayotoa huduma zake mpaka ngazi ya chini na ni lazima wawafikie wananchi na kuondoa malalamiko ya mara kwa mara yanayojitokeza.

Katika kuwafikia wananchi wengi zaidi ni lazima wahakikishe wanaimarisha zaidi matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ili wananchi kutoka maeneo mbalimbali waweze kupata huduma bila kufika Ofisi za Wakala na kuzipata kwa haraka na kwa gharama nafuu huko waliko.

Aliahidi suala la utoaji wa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu litakuwa moja ya mambo ya msingi watakayosimamia.

Ofisa huyo anasema anafahamu kuna mfumo wa eRITA ambao wananchi wanautumia kutuma maombi ya huduma na kuwataka wataalamu kuufanyia tathmini ili kubaini kama yatahitajika maboresho ili uweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na ifike wakati maombi yote yawe yanatumwa na kujibiwa kidijitali.

Watumishi pia wametakiwa kuzifahamu na kuziishi dira na dhima za taasisi ambazo zinasimama katika misingi ya kulinda haki na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazowaongoza.

Watumishi wanakumbushwa kutunza siri za ofisi, kuwa na nidhamu ya hali ya juu, kutumia lugha zenye staha ili wananchi wanaridhike na huduma zinazotolewa na wakala.

Wamekumbushwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu kwa kuwa wapo hapo kuwahudumia wananchi.

Pia wameahidiwa kutambuliwa na wamepongezwa watumishi wanaofanya kazi kwa bidii na kuvuka malengo, kwa kuahidiwa ushirikiano na kufanya kazi kwa uwazi ili kuleta umoja katika taasisi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi tawi la RITA, aliwataka watumishi kuwapa ushirikiano viongozi hao wapya na kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza malengo ya wakala.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## *Migogoro namna hii kwenye ardhi inapaswa kudhibitiwa, kila inapotokea*

Na Faustine Feliciane

**MWANZONI** mwa wiki hii, Waziri wa Ardhi, Anjeline Mabula, alitangaza serikali kuvalia njuga suala la migogoro ya ardhi na kuitokomeza kabisa hapa nchini. Ni jambo jema na lenye afya kwa umma wote wa Kitanzania, kiuchumi na kijamii.

Migogoro mingi inayotokea kuhusu ardhi, inachangiwa kwa kiasi kikubwa na utata wa kimaamuzi na hasa kwa waliopewa dhamana, hususan katika ngazi za hamashauri nchini.

Najua, ipo migogoro ambayo ama kwa asili au muundo wake inatatulika kirahisi na mapema, hata kuepuka kero zisizokuwa za lazima. Kwa mfano, mkoani Dar es Salaam katika Manispaa yake ya Kigamboni, kumekuwapo migogoro mingi ya ardhi, ambayo imedumu kwa muda mrefu.

Moja ya migogoro hiyo, ni ule unaotajwa katika kata ya Kimbiji kijiji cha Mikenge, ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 15. Mgogoro huo unatokana na uwekezaji wa kampuni mojawapo, ikidaiwa imeziba barabara inayoenda ufukweni, ambayo ilikuwa ikitumiwa na wakazi wa maeneo hayo, pamoja na wawekezaji wengine kufika katika maeneo yao.

Kimsingi, mgogoro huo umewagawa wananchi na ninaamini ulikuwa una sifa ya kutatuliwa na uongozi wa manispaa hiyo, bila hata ya kuchukua muda mrefu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliyepita, Amos Makalla, hata kuna wakati akaitisha kikao cha kuiingilia jambo hilo, alichukua hatua ya kuandaa mkutano wa pamoja mnamo Desemba mwaka jana. Ni katika mkutano huo, pia ukahusisha wataalamu wa ardhi wa Manispaa na mkoa lengo, ikiwa kuhitimisha mgogoro huo.

Hata hivyo, juhudi hizo pamoja na ushauri wa wataalamu wa ardhi tulioushuhudia na kutarajia ndio mwelekeo, tunaona uongozi wa juu wa wilaya hiyo, sasa umekuja uamuzi ambao nao unaibua mjadala mpya kwa wakazi wa eneo hilo.

> **Mwenyekiti serikali ya mtaa eneo hilo, Lameck Mayala, alinukuliwa katika kauli ya kusikitikia maamuzi hayo mapya, binafsi akiwa na mtazamo wa kupendelea zaidi uamuzi wa awali.**

Kwa mgogoro huo, kuna malalamiko ya wakazi wa mahali hapo kutofurahia kuanzishwa barabara nyingine, tofauti na mwelekeo wa uamuzi uliotolewa awali kuhusu suala hilo.

Eneo ambalo imeamuliwa barabara hiyo mpya ipite sasa kuwawezesha wananchi kufika ufukweni na wawekezaji wengine kufika kwenye maeneo yao, kuna korongo kubwa ambalo si rahisi kuwapo barabara sahihi.

Uamuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa - Makalla, ulikuwa na tija na kwa maono yangu, ulikuwa wa afya zaidi kama ungetekelezwa.

Hiyo ni kwa sababu, ikizingatiwa tayari taratibu mbalimbali za kutwaa sehemu ya ardhi hiyo yenye mgogoro zilikuwa zimeanza kuchukuliwa.

Mwenyekiti serikali ya mtaa eneo hilo, Lameck Mayala, alinukuliwa katika kauli ya kusikitikia maamuzi hayo mapya, binafsi akiwa na mtazamo wa kupendelea zaidi uamuzi wa awali.

Mwenyekiti huyo aliendа mbali zaidi, akiomba kuamuliwe anachokiita chenye tija zaidi kijamii. Nikirejea kauli ya Waziri Mabula, ni wazi serikali inataka kuvalia njuga migogoro ya ardhi hapa nchini, akiomba watendaji wengine waunge mkono jambo hilo na kutatua migogoro kwa manufaa ya wananchi.

Ni wazi Waziri Mabula ambaye naamini anaufahamu mgogoro huo wa Kimbiji, anaweza kurushia jicho na hata kuja na uamuzi wenye afya kwa pande zote mbili za mgogoro kuua malalamiko, huku katika matokeo hayo wananchi wanapaswa kufurahia uwapo wa fukwe za bahari na kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kama kawaida.

HABARI KITAIFA

## RITA: Watumishi ongezeni bidii kuhudumia wananchi

**Na Romana Mallya**

KABIDHI Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), Frank Kanyusi, amewataka watumishi kujipanga ili kuwafikia wananchi wanaohitaji huduma na kuondoa malalamiko yanayojitokeza mara kwa mara.

Ijumaa iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akiwaapisha wateule wake akiwamo Kanyusi pamoja na Naibu wake, Kabidhi Wasii Mkuu, Irene Lesulie, alitaja sababu ya kuwatumbua waliokuwapo kwenye nafasi hiyo kuwa ni kutokutekelezwa kwa kazi vizuri na ugomvi.

Akizungumza katika kikao cha wafanyakazi wa RITA baada ya kuanza kazi, Kanyusi aliwataka wafanye kazi kwa ushirikiano, umoja na upendo ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao na kuwawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi wanaowahudumia.

Aliwakumbusha kuwa RITA ni taasisi nyeti inayotoa huduma zake mpaka ngazi ya chini na kwamba ni lazima wawafikie wananchi na kuondoa malalamiko ya mara kwa mara yanayojitokeza.

"Ili kuwafikia wananchi wengi zaidi ni lazima tuhakikishe tunaimarisha zaidi matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ambapo wananchi kutoka maeneo mbalimbali waweze kupata huduma bila kufika ofisi za wakala na kuzipata kwa haraka na kwa gharama nafuu," alisema.

Kanyusi alisema suala la utoaji wa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu litakuwa moja ya mambo ya msingi watakayosimamia kikamilifu katika uongozi wao.

Pia alisema anafahamu kuna mfumo wa eRITA ambao wananchi wanautumia kutuma maombi ya huduma na watakaa na wataalamu na kuufanyia tathmini ili kubaini iwapo yatahitajika maboresho yanayotakiwa ili uweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na ifike wakati maombi yote yawe yanatumwa na kujibiwa kidijitali.

Naibu wake, Lesulie amewataka watumishi kuzifahamu na kuziishi dira na dhima za taasisi ambazo zinasimama katika misingi ya kulinda haki na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazowaongoza.

Alisema watumishi wanatakiwa kutunza siri za ofisi, kuwa na nidhamu ya hali ya juu, kutumia lugha zenye staha ili kuhakikisha wananchi wanaridhika na huduma zinazotolewa na wakala.

"Inabidi tuache kufanya kazi kwa mazoea na tuwe wabunifu katika utekelezaji wa majukumu kwani tuko hapa kuwahudumia wananchi. Ninaahidi kwamba, tutaendelea kuwatambua na kuwapongeza watumishi wanaofanya kazi kwa bidii na kuvuka malengo, nasi tunaahidi ushirikiano na tutafanya kazi kwa uwazi ili kuleta umoja katika taasisi," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi tawi la RITA, Adam Nkolabigawa, aliwataka watumishi kupewa ushirikiano viongozi hao wapya na kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza malengo ya wakala.




Wafanyakazi wa Bohari ya Dawa (MSD), wakifanya kazi ya kuhesabu mali kwa mujibu wa sheria. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni ili kuanza mwaka mpya wa fedha. Katika kipindi hiki maghala yote ya MSD makao makuu pamoja na kanda zote yatakuwa yamefungwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi bilioni 300/- zatumika kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema imetumia Sh. bilioni 393 katika sekta mbalimbali kwa mwaka kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwataka wananchi kutunza mazingira ili kuokoa fedha hizo.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Andrew Komba, wakati wa warsha ya kujenga uelewa wa kanuni na mwongozo wa biashara ya kaboni kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini.

Alisema bajeti ya serikali ya 2022/23 ilitenga Sh. bilioni 393.2 kutumika katika mapambano ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema serikali inapoteza fedha nyingi kutatua matatizo ya mabadiliko ya tabianchi na endapo mazingira yasipoharibiwa kuna uwezekano wa kuokoa fedha hizo.

"Kimsingi serikali inatumia fedha nyingi za ndani, lakini tuna miradi ya serikali ambayo inatekelezwa hapa nchini ikiwamo wa Sh. bilioni 4.6 kwa kujenga kuta za kuzuia mmomonyoko ya ardhi katika maeneo ya fukwe," alisema Komba.

**Pamoja na changmoto zinazochangiwa na mabadiliko ya tabianchi kumekuwa na fursa na jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo.**

Aidha, alisema kwa sasa wanazungumza mara kwa mara masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa sababu Tanzania hali siyo nzuri.

"Tunapata madhara makubwa yanasosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa maana ya kuongezeka kwa nyuzi joto katika uso wa dunia miaka ya nyuma hali ya hewa na sasa joto limeongezeka na linapoongezeka linaleta mabadiliko katika mifumo ya hali ya hewa," alisema.

Alisema nchi imeonekana katika maeneo hayo kufanya vibaya kwa kutumia rasilimali za ukataji miti kwa shughuli za kutengeneza nishati ya kupika.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Abdallah Hassan, alisema lengo kubwa la warsha hiyo ni kuwajengea uelewa wahariri wa vyombo vya habari ili kuelewa kanuni na mwongozo wa usimamizi na udhibiti wa biashara ya kanuni ya kaboni za mwaka 2022.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa isiyotabilika, ongezeko la joto, ukame na mafuriko.

Hassan alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zimeathiri sekta za kijamii na kiuchumi.

"Pamoja na changmoto zinazochangiwa na mabadiliko ya tabianchi kumekuwa na fursa na jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo," alisema.

Alisema serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni mapitio ya sera, uandaaji wa kanuni, mikakati na mwongozo ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, Hassan alisema biashara ya kaboni ni mojawapo ya nyezo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani.

Alisema serikali imeandaa kanuni na mwongozo wa taifa wa usimamizi wa biashara ya kaboni kwa ajili ya kuweka utaratibu na masharti ambayo wadau na wawekezaji wa biashara hiyo watapaswa kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi mipya na inayoendelea.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Mitazamo tofauti yazidi kusikika sakata Bandari

**Na Waandishi Wetu**

SAKATA la mkataba wa uendelezaji na uboreshaji wa bandari baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai, limemuibua Prof. Ibrahim Lipumba, akiitaka serikali kupokea ushauri wa wanasheria huku taasisi sita za kiraia, zikisisitiza uwekezaji huo ni muhimu.

Akizungumzia sakata hiyo jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, aliitaka serikali kuwa wazi na kupokea ushauri kutoka kwa wanasheria ni lipi la kufanya kurekebisha matatizo yaliyojitokeza kwenye mkataba huo.

"Mjadala huu umechukua nafasi kubwa na hata kuweza kughubika mjadala wa bajeti ya serikali. Ni muhimu kwa serikali kuwa wazi katika suala hili.

"Ukosefu wa uwazi unasababisha sintofahamu ambazo tayari zinatumiwa kutugawa. Makosa yakifanyika ni bora kukubali na kuyarekebisha," alisema Prof. Lipumba ambaye ni mbobezi wa uchumi huku akiainisha mapungufu saba ndani ya mkataba huo.

Pia alisema baadhi ya vifungu vya Mkataba hasa 7(3) na 23(4) vinaweza kutafsiriwa kuwa vinaingilia uhuru wa Tanzania kufanya maamuzi yake ya kimsingi.

Kadhalika, alisema Bunge lilikuwa na fursa ya kuisadia serikali kurekebisha kasoro zilizojitokeza kabla ya kuridhia mkataba huo.

Prof. Lipumba alisema kwa madhumuni ya kuboresha utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam hapakuwa na sababu ya kuwa na mkataba baina ya nchi bali na Mamlaka ya Banadari Tanzania (TPA) kwa njia ya zabuni ya ushindani wa wazi.

Wakati Prof. Lipumba akisema hayo, taasisi sita za kiraia zimeungana na kusema, uwekezaji ambao serikali unataka kufanya ni muhimu na kusisitiza kwamba, imefika wakati Tanzania kuinuka kiuchumi na kushindana na mataifa makubwa kibiashara.

Taasisi hizo ni Tafeyoco Tanzania, Taifa Trust, Seft kwanza, Wazalendo halisi, Cawo connect na Tanzania Society Civil Organization.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya Tafeyoco Tanzania, Elvice Makumbo, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema wanataka Watanzania kuwa makini na watu wanaopotosha suala hilo.

"Suala la bandari ni vita vya kiuchumi kuna watu wanatumiwa kuhujumu nchi kwa maslahi yao binafsi. Anachokifanya Rais Samia Suluhu Hassan ni uthubutu kwa ajili ya faida ya Mtanzania na taifa kwa ujumla, hivyo tuache kusikiliza upotoshaji unaofanywa.

"Mkataba wa bandari na kampuni ya DP World siyo jambo la wanasiasa tu au viongozi wa dini ni la watanzania wote kwa sababu linahusu rasilimali za nchi. Kila Mtanzania ana haki na wajibu wa kutoa maoni yake katika njia sahihi, tusilifanye kuwa kichaka cha kupenyeza mambo yetu ya kisiasa," walisisitiza.

Walidai kwamba, upotoshaji unaoendelea ni kuleta taharuki na kushauri kuwa, ifike mahali uzalendo uwe sehemu ya maisha na kuacha ubinafsi wa kisiasa.

Mtaalamu wa masuala ya maadili kutoa Taasisi ya Taifa Trust, Romvald Rwechungura, alisema, "wote wanaopinga jitihada zinazofanywa na serikali wanakabiliwa na tatizo la uelewa mdogo.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, katika andiko lake lililopo mtandaoni, amechambua kinachoendelea akiangazia maeneo 10 yanayotajwa ambayo ni rushwa, umoja na utaifa, udini na siasa, ujuzi wa sheria na uchumi, Bunge na serikali.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Maulid Mmbaga**

# AMDT yainua kiuchumi wanawake wajasiriamali

**Na Maulid Mmbaga**

WANAWAKE mkoani Dodoma wanaojihusisha na kilimo na ujasiriamali wamepiga hatua kiuchumi na kubadilisha maisha yao baada ya kuwezeshwa kielimu, mtaji na vifaa vya kisasa vilivyowasaidia kuongeza ufanisi wa viwanda vya usindikaji wa mafuta ya alizeti.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni mkoani Dodoma, Meneja wa mradi unaohamasisha kilimo chenye tija kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Kilimo Denmark Asia (ADDA Tanzania), Mercy Kingo, alisema wanafanya kazi kwenye mradi huo unaofadhiliwa na Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT).

Alibainisha kuwa wajasiriamali hao wanakabiliwa na changamoto ya kukosa mitaji na uwezo wa kusimamia na kuendesha viwanda vidogo, ambazo zimetatuliwa kwa kushirikiana na AMDT, ADDA Tanzania.

"Tunahakikisha kinamama wanakuwa na uwezo wa kutunza taarifa zao, waone faida ya kinachoingia na kutoka katika biashara wanayoifanya, pamoja na kuhakikisha viwanda na mitambo wanayoitumia katika usindikaji wa alizeti inakuwa ya kisasa ili watoe mafuta yenye ubora," alisema na kuongeza;

"Katika kufanikisha hilo mradi unatoa asilimia 60 katika kununua mashine nzuri na bora na wenyewe wanatoa asilimia 40 ya fedha, pia tunawasaidia kuhakikisha bidhaa wanazozizalisha zinapata masoko na kufahamika," alisema Mercy.

Alieleza kuwa wanawasaidia pia kupata vibali kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na kuhakikisha miundombinu ya mahali wanapofanyia kazi inaendana na matakwa ya shirika hilo.

Aidha, alibainisha kuwa wanafanya kazi pia na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), kuhakiki viwango vya bidhaa wanazozalisha na kwamba wanashirikiana pia na Shirika la Brazil la utoaji wa huduma za kijamii viwandani (SESI) kwa ajili ya kuwapatia mafunzo.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 28/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | ALEX MATHEW MWAIPYANA | NYUMBA | ALEX MATHEW MWAIPYANA | KINYEREZI-ILALA | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | DICKSON CHRISTIAN NGEMELA | NYUMBA | DICKSON C. NGEMELA | KIMARA TEMBONI | 06/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | YAHYA OMARY MTORO | NYUMBA | YAHYA OMARY MTORO | VIANZI-VIKINDU | 11/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | OMARI SAIDI OMARI | NYUMBA | MIZE MASOUD HASSAN | MIKWAMBWE-KIGAMBONI | 18/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | BUNDALA SOSELA NDUNGUMIKA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | BUNDALA SOSELA NDUNGUMIKA | BUYUNI-CHANIKA | 13/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | NESTORY REVOCATUS NJAU | NYUMBA | NESTORY REVOCATUS NJAU | MVUTI-ILALA | 13/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SALIM SULEIMAN HEMED | NYUMBA | SALIM SULEIMAN HEMED | MKURANGA | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SELEMAN YUSUPH MAGANGA | NYUMBA | SELEMAN YUSUPH MAGANGA | MPONDA-MIANZINI | 14/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SULEIMAN HAMZA MGAGI | NYUMBA (2) | SULEIMAN HAMZA MGAGI | 1.KISEMVULE -MKURANGA 2.BUNGU-RUFIJ | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | GLORY SUMUN MASSAWE | NYUMBA | GLORY SUMUN MASSAWE | ULONGONI-ILALA | 13/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0715868000/0712667989**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



# Mabadiliko tabianchi chanzo migogoro katika jamii

**Na Mary Mosha,** SAME

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2023, Abdalah Shaibu Kaim, amesema migogoro mingi kati ya binadamu na wanyamapori, wafugaji na wakulima, inachochewa na hali mbaya ya mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea hivi sasa nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, baada ya kuweka jiwe la msingi kitalu cha miti kinachomilikiwa na Wakala wa Misitu Nchini (TFS), Kanda ya Kaskazini.

"Ajenda ya utunzaji wa mazingira na upandaji wa miti ni mkakati wa kitaifa. Ni mkakati ambao kila mwananchi anapaswa kuuzingatia ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Ndiyo maana katika siku za hivi karibuni, kumesikika kilio cha kukosekana kwa maji, migogoro ya wafugaji na wakulima na ukame. Hii yote ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo kila mmoja ahakikishe anapanda miti na kuitunza," alisema.

Awali, Ofisa Tawala wa TFS, Benard Mghweno, alimweleza kiongozi hiyo wa mbio za Mwenge kitaifa, kwamba tangu kuanzishwa kwa bustani hiyo kati ya mwaka 2017/18, imezalisha miche ya miti mbalimbali 2, 560, 000 kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Same.

Alisema: "Kati ya mwaka 2020 hadi 2023, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, TFS imefanikiwa kupanda jumla ya miti milioni 1, 405,478. Miti hiyo imepandwa katika hekta 700, sawa na asilimia 93.7 ya lengo la mwaka, ambalo ni kupanda miti milioni 1.5".

Zaidi aliongeza: "Miti hii imepandwa maeneo ya wazi ya taasisi binafsi na serikali, mashirika ya dini, mashambani, katika vilele vya milima na hifadhi na makazi ya watu. Tayari miti 24,655 imeoteshwa kwenye vyanzo vya maji 12, ikiwamo Yangoma, Nakombo, Kigwerere na Pangani".

Kwa mujibu Mghweno, kwa kipindi cha Juni hadi Julai, jumla ya miti 900,000 imegawanywa kwa shule za msingi na sekondari, asasi za kiraia ambazo ziligawa miti 773,000.

# Wawekezaji sekta ya viwandani wakumbushwa kuzingatia sheria

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAWEKEZAJI wa sekta ya viwanda, wamepewa sharti la kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali ya kazi nchini, ikiwamo kuboresha mifumo ya usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi ili kulinda wafanyakazi dhidi ya athari wanazoweza kuzipata wakiwa kazini.

Jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, aliwapa somo hilo wawekezaji, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kutembelea viwanda mkoani Arusha.

Kamati hiyo ilikwenda kujionea utekelezaji wa sheria na miongozi mbalimbali ya kazi, ikiwamo Sheria Namba 5 ya Usalama na Afya, Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003.

"Tunapenda wawekezaji waje nchini kwa wingi na wanapowekeza basi waendeshe shughuli zao zote kwa kuzingatia sheria mbalimbali za nchi. Huwa tunafurahi sana tunapoona wawekezaji wanatengeneza ajira kwa vijana wetu, lakini wakiendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema Prof. Ndalichako.

**Kamati hiyo ilikwenda kujionea utekelezaji wa sheria na miongozi mbalimbali ya kazi, ikiwamo Sheria Namba 5 ya Usalama na Afya, Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003.**

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Riziki Lulida, aliwasihi wawekezaji hao kuhakikisha wanaweka miundombinu rafiki katika maeneo mbalimbali ya viwanda vyao, kwa ajili ya jamii ya watu wenye ulemavu.

"Tunazo sheria za nchi zinazoelekeza viwanda kujenga miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kwa mfano mimi leo nimeshindwa kuingia ndani katika baadhi ya viwanda tulivyotembelea kutokana na ulemavu wangu wa miguu. Hii ni kwa sababu maeneo mengi yana ngazi, naamini kuna wafanyabiashara wengi wenye ulemavu, ambao pengine wanatamani kuingia katika maeneo ya viwanda na wakashindwa," alieleza.

Mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Jang'ombe, Ali Hassan King, ameishauri Wakala wa Usalama na Afya, Mahali pa Kazi (OSHA), kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa usalama na afya katika maeneo ya kazi nchini, huku akiahidi kuwa wataendelea kuishauri serikali juu ya uimarishaji wa mifumo ya usalama na afya katika viwanda.

Baada ya kauli hizo, Mkurugenzi wa OSHA, Dk. Jerome Materu, alisema kuwa kuna umuhimu mkubwa sana kwa wawekezaji wote kuzingatia taratibu na miongozo yote ya usalama na afya kwa sababu huongeza tija na kupunguza gharama za uendeshaji wa maeneo yao ya kazi.

Aidha, wawakilishi wa viwanda vilivyotembelewa wameishukuru kamati hiyo kubainisha kuwa ziara hiyo imewapa funzo kubwa huku wakiahidi kuendelea kuboresha zaidi mifumo ya usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi.

Katika ziara hiyo Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendelea ya Jamii imetembelea viwanda vitatu mkoani Arusha ambavyo ni Kiwanda cha Kuzalisha Transifoma cha TANELEC Limited, Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa mbalimbali ikiwamo nguo cha A to Z Textiles Mills Ltd na Kiwanda cha Maua cha Fides Tanzania.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akisalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Heri James, baada ya kuwasili kwenye kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za serikali katika kipindi cha mwaka 2021/22 ambapo alimpongeza mkuu huyo kwa kusimamia halmashauri hiyo na kupata hati safi. **PICHA: MARY MARGWE**



# Samia mgeni rasmi Siku ya Dawa za Kulevya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Dawa za Kulevya Duniani, ambayo kitaifa yatafanyika mkoani Arusha, Juni 25 mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema jana kuwa Rais Samia, atafungua maonyesho hayo ambayo yatatanguliwa na maonyesho ya shughuli za dawa za kulevya yatakayoanza Juni 23.

Kwa mujibu wa Mongela, dawa za kulevya zimeacha athari kubwa kwa vijana, ambao ni nguvu kazi ya taifa, hivyo ameshauri ni vyema kila mtu akashiriki kupinga matumizi na biashara hiyo.

Akizungumza jana jijini Arusha na waandishi wa habari, Mongella, alisema maadhimisho hayo yatafanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Maadhimisho hayo yanaongozwa na kauli mbiu isemayo, 'zingatia utu, imarisha huduma za kinga na tiba' yana lengo la kuhakikisha kila jamii ipige vita dawa za kulevya.

"Athari hizi zinarudisha nyuma maendeleo ikiwamo uchumi wa familia, hivyo wadau wote tuungane na serikali kupiga vita matumizi na biashara ya dawa za kulevya,"alisema.

Vilevile, aliomba viongozi na jamii kuwajibika, ili kudhibiti janga la matumizi ya dawa za kulevya na kila mmoja achukue hatua za kupiga vita matumizi na biashara hiyo.

Alisema dawa hizo zinasababisha baadhi yao kujiingiza katika uhalifu na kuleta adha kwa baadhi ya jamii, hivyo muhimu kila mmoja kupiga vita matumizi ya dawa hizo.

Mongella alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya na kazi kubwa ya kuanzisha vituo vya urekebishaji kwa waathirika wa dawa za kulevya.



# 16,000 wanolewa elimu ufuatiliaji matumizi rasilimali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI zaidi ya 16,000 kutoka kata sita mkoani Shinyanga, wamefikiwa na kupewa elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya uboreshaji huduma za kilimo (PETS).

Lengo ni kuongeza uzalishaji wa chakula na biashara ili kukabiliana na tishio la njaa.

Wananchi hao wanaotokea katika Kata ya Tinde, Didia, Nyandekwa, Igunda, Kinamapula na Bukomela wamepata mafunzo hayo kutoa Chama cha Watu Wasioona mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la FCS kwa Sh. milioni 43.9.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu juzi, Mwenyekiti wa chama hicho, Marco Nkanjiwa, alisema mradi huo umekuwa msaada kwa wananchi na wakulima hususani katika kuongeza viwango vya uzalishaji wa mazao ya chakula na kuweka akiba.

**Mradi huo umekuwa msaada kwa wananchi na wakulima hususani katika kuongeza viwango vya uzalishaji wa mazao ya chakula na kuweka akiba.**

Alisema kabla ya kuwafikia na kuwapatia elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma walikuwa hawafahamu namna ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo na wapi wanatakiwa kuzifuatilia kwa lengo la kuzalisha mavuno.

Alisema kwa sasa wanafahamu na wamezalisha zaidi mazao ya chakula na biashara.

Mmoja wa wakazi wa Nyandekwa Manispaa ya Kahama, Eva Machanya, alisema ili kuzalisha kwa tija na kupata mavuno mengi maofisa ugani wanapaswa kuhakikisha wanawatembelea mara kwa mara na kutoa ushauri juu ya aina gani ya mazao kulingana na eneo husika na nyakati zilizopo.

Naye Evaristi Masanja alisema serikali inatakiwa kuyafufua mashamba darasa na umwagiliaji yaliyokuwa yakitumika katika kuwafundisha wakulima namna ya kulima kwa tija ili kuendelea kuongeza uelewa wa uzalishaji chakula kama ilivyokuwa awali.

Pia, aliiomba serikali kwa kushirikiana na maofisa ugani waliopo katani kuwadhibiti wanunuzi wanaofika shambani moja kwa moja na kuwarubuni wakulima kuuza mazao yakiwa bado hajakomaa.

Alisema ili kuondoa hilo inatakiwa kuyadhibiti masoko holela kwanza yanayofanywa na wanunuzi.

# Halmashauri ya Maswa yatatua hoja 66 za CAG

**NaAlex Sayi,** MASWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu imefanikisha kutatua na kuzipatia ufumbuzi hoja 66 kati ya 98 zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), huku hoja 32 zikiwa kwenye hatua ya utekelezaji.

Hayo yamebainishwa juzi na Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Hesabu za Serikali za Mitaa Mkoa wa Simiyu (CEA), Gwamaka Mwakyosi, kwenye baraza maalumu la madiwani la kujibu hoja za CAG lililofanyika katika halmashauri hiyo.

"Licha ya halmashauri hii kupata hati safi kwa mwaka wa ukaguzi 2021/2022 hata hivyo ilikuwa na hoja za kujibu 98 na kati ya hizo hoja 66 zimejibiwa na zimefungwa nakusaliwa na hoja 32 ambazo zipo kwenye hatua ya utekelezaji," alisema Mwakyosi.

Kuhusu hoja za mifuko ya Afya ya Jamii (HBF), alieleza kuwa halmashauri hiyo imefunga hoja nane kati ya hoja 10 (80%) na kusaliwa na hoja mbili sawa na asilimia 20, huku hoja nne zinazohusisha mfuko wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu zikiwa kwenye utekelezaji wa asilimia mia.

"Halmashauri ilipokea hoja nne toka Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAC), tayari hoja tatu zimetekelezwa, huku hoja 50 za CAG za muda mrefu toka mwaka 2015/2021, hoja 41 kati ya hizo sawa na 82% zimefungwa na kusaliwa na hoja tisa sawa na 18%," alieleza Mwakyosi.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, akizungumza kwenye baraza hilo aliwataka wataalamu na wakuu wa idara wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanatimiza majukumu yao kwa mujibu wa miongozo ya kiutumishi na siyo kuisababishia hasara halmashauri.

Aliongeza kusema kuwa hatapenda kuona halmashauri hiyo inaongeza hoja za kujibu kwa CAG ambazo hazina maana yoyote na kuwaelekeza watumishi na wakuu wa idara kuhakikisha kuwa hawaisababishii hasara halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Maswa, Onesmo Makota, aliwataka watumishi na madiwani kuhakikisha wanasimamia fedha za maendeleo zinazoletwa na Rais Samia ili ziwe na matokeo chanya na kutatua matatizo yanayowakabili wananchi.

**Halmashauri ilipokea hoja nne toka Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAC), tayari hoja tatu zimetekelezwa, huku hoja 50 za CAG za muda mrefu toka mwaka 2015/2021, hoja 41 kati ya hizo sawa na 82% zimefungwa na kusaliwa na hoja tisa sawa na 18%.**

# Wenyeviti serikali za mitaa wakumbushwa majukumu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WENYEVITI wa serikali za mitaa mkoani Shinyanga wametakiwa kufanya mikutano ya hadhara mara kwa mara na kusikiliza kero za wananchi ikiwa ni pamoja na kuzitafutia ufumbuzi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa CCM Kata ya Mjini Manispaa ya Shinyanga na kusema kuwa juhudi zao katika kuwahudumia wananchi ndiyo yatakuwa malipo yao mwaka 2024.

Alisema lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanafikiwa kwa wakati na viongozi hao wanatekeleza wajibu wao.

Alieleza kuwa uaminifu kwa wananchi unajengwa kwa kuwafikia na kusikiliza kero walizo nazo wananchi hao na kuhakikisha wanazitatua kwa wakati kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi zingine.

"Hii ni pamoja na viongozi wa CCM kuanzia ngazi ya matawi, tatueni kero za wananchi kupitia mikutano ya hadhara, ili uchaguzi ukifika mwakani iwasaidie ninyi pamoja na chama kwa ujumla,"alisema Mlolwa.

Aidha, aliwasihi viongozi hao kuwa wakati wa mikutano yao ya hadhara kwa wananchi waitangaze pia na miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa kwao na kuendelea kumuunga mkono Rais Samia kwa kuitunza miradi hiyo ili kero zilizodhibitiwa zisijirudie tena.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, aliwataka viongozi wa chama kuanzia ngazi ya matawi kujipanga vyema katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani pamoja na kufanya vikao ili kuhakikisha wagombea wote wa CCM wanapata kura nyingi na kushinda.





Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 60 walizozikamata katika doria walioifanya ndani ya mwezi mmoja, ikiwamo na mirungi bunda 58. **PICHA: MARCO MADUHU**

ama
ALHAMISI JUNI 22, 2023
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## DC Jokate abuni mbio za wajawazito zenye washiriki 2000, zilivyotia fora




## Waziri Makamba: Hii hapa mikakati rasmi kupata umeme wa jotoardhi

Ukurasa 14

# Vita Mazingira vya Rais, mchanganuo wake unavyojitokeza kwenye bajeti

## •Dola milioni 33.9 mezani ya miradi mikakati

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa Dodoma**



Aina ya matunzo duni ya kimazingira, ambayo serikali sasa inachukua hatua za kibajeti kukabili. **PICHA: MTANDAO.**

TANZANIA kama zilivyo nchi nyingine inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri uchumi wake, ikiwamo kwenye uzalishaji wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na utalii.

Ni alhamisi ya wiki iliyopita, bungeni kuliwasilishwa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali, ambayo sasa yanaendelea kujadiliwa, ikibeba msimamo na mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhusu anachonuia kuwatekelezea wananchi kitaifa, kwa huduma na maendeleo.

Msingi wa bajeti nzima ni mustakabali kwa kila tendo kiserikali kwa taifa, ndani yake kukiwapo eneo la mazingira, ambalo tangu aingie madarakani, Rais Dk. Samia amekuwa akipigania maboresho yake, kwa kushirikisha sekta binafsi.

Uwasilishi wa bajeti unaoendelea kujadiliwa sasa, una maana kubwa kutafsiri uwasilishi wa Rais na miaka yake miwili madarakani, akikutana na kujadili na makundi kadhaa, yakiwamo ya kidini kuhusu mwelekeo wa kuhifadhi mazingira na tabianchi nchini.

Ikirejewa Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Dk. Samia iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, mteule wake madarakani kwa miaka miwili ya nafasi hiyo, imegusa sana mazingira.

Kwa mujibu wa uwasilisho huo, Waziri wa Fedha kwenye sekta mazingira, amegusa zaidi: Kilimo cha umwagiliaji; utekekezaji Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 kuhusu mazingira; ushuru kwa magari ya abiria yenye umri unaozidi miaka mitano na Programu ya Nishati Safi, sababu kuu anataja nchi inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sehemu kubwa.

Ni uwasilisho uliosomwa muda mmoja ndani ya nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kila Waziri wa Fedha mhusika akiwasilisha mwelekeo wa kiuchumi wa serikali ya rais aliyeko madarakani sasa.

### NDANI YA BAJETI

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu, anasema serikali ya Rais Dk. Samia inaendelea kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) unaojumuisha kilimo cha umwagiliaji, ambao undani wake waliutoa mawaziri wenye dhamana na kilimo, pia mazingira.

Sura nyingine, waziri anaitaja Tanzania ikiwa mwanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), inachukua hatua kutekeleza Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 unaohusu kupunguza asilimia 30 hadi 35 ya gesi joto inayotoa.

Anataja kupitia Mchango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC) hadi mwaka 2030, Dk. Mwigulu anafafanua Mfuko wa Global Environmental Facility, Tanzania ni mwanachama na imeitengewa Dola za Marekani milioni 33.59 za miradi ya kusimamia mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kwa kipindi cha miaka minne, unaokamilika hadi mwaka wa fedha 2025/26.

Akibeba wajibu wa rais bungeni,Dk, Mwigulu anawakumbusha mawaziri husika wa sekta za mazingira na mabadiliko ya tabianchi, waandae miradi sahihi, ili wanufaike na fedha hizo.

Anafafanua: "serikali inaendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo ili kuongeza fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi,"

Dk. Mwigulu anapendekeza kutozwa ushuru wa bidhaa kwa asilimia 10 kwenye magari ya abiria yanayoingizwa nchini yanayozidi umri wa miaka mitano (magari chakavu), huku kukifutwa ushuru wa forodha kwa mabasi ya abiria kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Vilevile anapendekeza kutozwa ushuru wa bidhaa za magari asilimia tano, kwenye magari yenye uwezo wa injini kati ya lita za ujazo 1000 hadi 2000 na kutoza ushuru asilimia 10 kwenye magari yenye uwezo lita za ujazo 2000.

Vilevile anapendekeza kutengwa bajeti ya utekelezaji wa Programu ya Nishati Safi, Sh. bilioni 4.5 zitakazotumika katika hatua za awali, ikiwamo maandalizi ya uratibu, uhamasishaji na elimu kwa wananchi, mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu nishati safi.

Pia, anataja kumeongezwa tozo za nepi za kigeni, ambazo nazo taka zake huzagaa mitaani.

### MAONI YA WADAU

Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira, Sara Pima, anasema pesa hizo ni muhimu nchini kwenye kusaidia Watanzania kukabiliana na athari za mazingira.

"Barabara zinapokuwa mbovu zinasababisha hasara kubwa kwa mkulima, wakati mwingine mazao yanachelewa kufika sokoni kwa

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# DC Jokate abuni mbio za wajawazito zenye washiriki 2000, zilivyotia fora

## •Wapagawa, hawakujali mvua; awaambia 'nimejifunza zaidi'

**Na Beatrice Shayo**

HILI wazo la mbio za wajawazito, nililibuni mwenyewe. Nikakaa na vijana fulani ambao wanafanya masuala ya lishe, nikashirikiana nao nini cha kufanya kwenye masuala ya wajawazito tangu nilivyokuwa mjamzito, nilikuwa na hili wazo," anatamka Mkuu wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Jokate Mwegelo.

Mbio hizo sasa kazibatiza jina la 'Mamathon' yenye kaulimbiu 'Mwendo wa Mama' zikafanyika Mei 28 mwaka huu kuanzia ofisini kwake, kuelekea kwenye viwanja vya Shule ya Msingi ya Mazoezi, lengo ni kutetea afya za wanawake.

Ni zaidi ya wajawazito 2,000 walijitokeza kushiriki mbio hizo Korogwe Vijijini walikuwa wajawazito 983 na Korogwe mjini wajawazito 1,223.

Matembezi hayo yakaibua mshangao, kwa kile kilichotajwa 'haijawahi kutokea' huku wahusika hao wakiwa na shangwe ya kutembea, bila ya kujali hali ya mvua iliyokuwa ikinyesha.

Mbio hizo zilibeba shangwe mbalimbali, Mkuu wa Wilaya Jokate, aliahidi kuwapatia zawadi kemkem wajawazito washiriki wa mbio hizo, ikiwamo vifaa vya kujifungulia, unga wa lishe, khanga na sabuni.

"Nilivyokuwa mjamzito nilijitahidi kuwa 'active' (kuchangamka) nilikuwa nasoma 'benefit' (manufaa) za kuwa 'active', wakati wa ujauzito. Hii huchangia kujifungua vizuri na kwa haraka na inasaidia kwenye afya ya mama na mtoto," anasema Jokate.

Anasimulia ujauzito una changamoto zilizomsababishia afikiri kuanzisha wazo hilo la kuwa na mbio mahsusi za wajawazito, akiwa na ufafanuzi: "Sikupata matatizo.. mwishoni nilipata 'presha' hiyo ilitokana na hali ya mimba ilivyo, ni zile presha za kutokana na ujauzito.

"Kutokana na hali ya kazi yangu, inanitaka muda mwingi niwe 'field' (penye kuwajibika) haikunilazimu kukaa, ilinipasa nifanye kazi niende mtaani, nikaona kuna umuhimu wa mwili kuwa 'active' unapokuwa mjamzito."

Jokate anasimulia ndani ya ujauzito wake, akagundua amekosa taarifa nyingi sahihi, baadaye akakutana na mtaalamu wa uzazi, aliyemueleza nafasi ya mazoezi maalumu wakati wa ujauzito, hata baada ya kujifungua.

"Si kila mazoezi unatakiwa kuyafanya wakati, naendelea kupambana kupata taarifa sahihi...nikapata wazo hili, inaweza ikawa ni fursa ya kuwaelimisha kinamama kufanya mazoezi kwa njia ya matembezi au mbio kwa wajawazito na kuwapatia elimu ya afya, lishe, elimu ya umuhimu kuhudhuria kliniki kwa wakati na elimu ya kuzingatia yale ambayo tunaelezwa kliniki,"anasema Jokate.




Kinamama wakishiriki mbio maalum za wajawazito wilayani Korogwe. **PICHA: BEATRICE SHAYO.**

### KISA CHA ZAWADI

Mkuu wa Wilaya huyo anasema wametoa zawadi za vifaa vya kujifungua, akizitaja kuwa ni khanga 1,000 na akaahidi vifaa vingine watapatiwa kwenye vituo vya afya, kwa ambao hawakupata vifaa hivyo.

"...'why delivery kit?'(kwanini vifaa vya kujifungua), kwa sababu unaweza kukuta mtu anaenda kujifungua hakuna vifaa, lakini tunavyotoa vifaa tunamhamasisha mama kwenda kliniki na kujifungua sehemu sahihi. Pia, tunaunga mkono juhudi ya kuwa na 'universal health' yaani afya kwa kila mwananchi kuanzia ngazi za chini," anasema Jokate.

Jokate anaeleza matarajio yake makubwa katika mbio hizo, ni kuokoa afya za wanawake na watoto kupunguza vifo vinavyotokana na ujauzito.

Mkuu wa Wilaya, anasema mbio za 'mamathon' zinalenga kuwahamasisha kinamama kuondoa dhana potofu wanazozipata wanapokuwa wajawazito.

Pia anaanika dira yake kwa mbio hizo zitakuwa endelevu, kuboresha wodi ya waangalizi wa watoto, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha maboresho ya miundombinu ilioko.

"Malengo mengine ni kuona kinamama wanahamasika kujifungua katika vituo vya afya, serikali inawekeza katika kuboresha miundombinu ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na rufani, zikiweka vifaa vya kisasa," anaeleza .

Jokate anasema majengo tajwa ya uzazi ni huduma mahsusi kwa kinamama watumie kwa matarajio, kinamama wataacha kujifungulia nyumbani, wakihamia kwenye vituo vya afya.

### HALI YA KOROGWE

Jokate anasema, wilayani Korogwe kunatajwa kinamama wengi wanajifungulia nyumbani, huku kukiwapo taarifa za mikasa ya wazazi kuwa na tatizo la kutupa watoto.

Anasema, kabla ya kuanza mbio alipata ushauri kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wataalamu na waganga wakuu wa hospitali ya wilaya, kwamba walijipanga namna ya kuwahudumia wajawazito watarajiwa kujitokeza kwenye mbio, sasa wakiiona kwa mafanikio.

"Kiukweli, wananchi wamepokea vizuri mbio wamekuja tukatembea nao pamoja hata mimi sikutegemea kama nitakutana na ule umati mliouona nimefarijika na jambo hili litakuwa endelevu tunahitaji uzazi salama na serikali yetu imekuwa ikipigia debe jambo hilo,"anasema

Jokate anayasifu mazoezi hayo ni mazuri, na kuwajenga wahusika wote kuimarika kimawazo, kuelekea kwenye wema na wengine.

### MASHARTI YA MBIO

Jokate anasema kuwapo mbio hizo, kuliwajulisha wajawazito wanaotakiwa mwisho ni wale wenye miezi sita, ingawa wakajitokeza wengine waliokuwa katika hatua ya kujifungua.

"Wapo waliokuja zaidi ya miezi sita hatukuweza kuwakataza, tayari wataalamu wetu wa afya walijipanga kuwahudumia," anasema Jokate.

"Unaweza ukasema hivyo lakini uamuzi unabaki kwa mtu binafsi. Wamekuja unawazuia vipi?" alitamka Jokate na anaendelea" Tulichokifanya, ni kujipanga kuwahudumia itakapohitajika huduma zaidi wapo wajawazito saba walipata dalili kama za uchungu walipelekwa hospitali wakaonekana, bado kidogo wakaruhusiwa kurudi nyumbani," anasema Jokate.

Anafafanua, akapata taarifa kuna wajawazito walizuiwa na waume zao kushiriki mbio hizo akinena: Wanaambiwa 'mnaenda kufanya nini kule', halafu kingine watu wanaona ujauzito kama ni tabia, yaani kufanya kazi ukiwa na mimba. Unaonekana kama ni jambo gumu, jambo ambalo halitakiwi katika jamii, wakati ni jambo la kawaida hiyo ndio 'process' (mchakato) wa uzazi."

Kwa mujibu wa Jokate, elimu inahitajika ili wananchi waondokane na dhana hiyo na kuna umuhimu wa mjamzito kufanya mazoezi.

### MAANA YA KAULIMBIU

Kaulimbiu tajwa zilikuwa na ujumbe wa 'Mwendo wa Mama', Mkuu wa Wilaya Jokate, akisema inatafsiri kwamba ni mwendo aliouanza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoongoza nchi.

"Hii kaulimbiu yetu ya 'mwendo wa mama' ni kutambua mchango wa Rais Samia jinsi anavyoitumikia Tanzania hususani alivyoligusa kundi la akina mama kwenye kila pembe na kila kona ya nchi," anasema.

### KINAMAMA NA UCHUMI

Jokate anasema, mbali na mbio hizo za wajawazito, anatamani kufanya suala la kiuchumi kwani alichokigundua kinamama ni lazima wawe vizuri kiuchumi, ili wamudu kuzingatia afya zao za uzazi, pia mtoto.

"Ni muhimu uwe na hela zako fulani hivi...bila kumsubiri sijui mwenza wako kuna vitu unavihitaji mpaka uje kuomba saa ngapi ukiwa na hela zako unajifanyia," anasema Jokate.

MAZINGIRA

# Taka plastiki shida, zachafua Ziwa Victoria zikidhuru viumbe waliomo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

Ni siku kadhaa tangu kumalizika Wiki ya Mazingira Duniani. Pia ni jana tu gazeti la Nipashe liliongozwa na habari, mabomba ya sindano kati ya uchafu unaokotwa kwa wingi ufukweni.

Ndani ya maadhimisho hayo ya Siku ya Mazingira Duniani, kunaripotiwa shughuli za kibinadamu zimeendelea kuwa kikwazo katika vita dhidi ya utupaji holela bidhaa za plastiki Ziwa Victoria, hata kuhatarisha uhai wa viumbe vilivyomo majini na nchi kavu.

Duniani kunatajwa kila dakika kuna chupa za plastiki za maji ya kunywa milioni moja zinanunuliwa, pia mifuko ya plastiki trilioni tano inayotumiwa kwa siku, inatumika kila mwaka na sehemu ndogo ndiyo zinarejeshwa kwa matumizi.

Utafiti uliofanywa na mwanazuoni na Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Bahati Mayoma, mwaka 2014, ukabaini asilimia 95 ya uchafu Ziwa Victoria, ni wa vipande vidogo vya plastiki.

Pia katika ngazi ya dunia, tani milioni nane za plastiki zinaishia bila kufanyiwa kazi.

Mwaka 2015, mwendelezo wa utafiti ukabaini vipande vya plastiki chini ya ziwa hilo ni zaidi ya tani 150, vilevile ukagundua wastani wa samaki mmoja kati ya watano wamemeza vipande hivyo, hali inayohatarisha uhai wa viumbe hivyo na binadamu wanaowatumia kitoweo.



Sehemu ya Mto Kanoni ulioko Bukoba unaotiririsha maji kwenye Ziwa Victoria. **PICHA: MTANDAO**

### ZIARA YA MIALO

Nipashe ilitembelea kwenye baadhi ya mialo mkoani Mwanza na kubaini uchafuzi wa Ziwa Victoria unaofanywa na wavuvi, pia wafanyabiashara katika mialo hiyo, sehemu kubwa ni uchafu uliojaa mifuko na chupa za plastiki.

Inatajwa kuwa hali inayosababishwa na ongezeko la watu eneo hilo lisilo na sehemu rasmi ya kumwaga taka. Pia kuna taka zinazosafiri mitaroni, maji yakitiririsha mkondo wake katika Ziwa Victoria, hivyo taka zote zinasombwa, zikiwamo plastiki na zinakusanywa ziwani, hata kusababisha miundombinu ya barabarani inaziba, zikichangia mafuriko barabarani.

Abdullahaziz Shabani, ni mvuvi katika Mwalo wa Mswahili, anasema wamekuwa wakikusanya taka jirani na ziwa, ila wingi wa wafanyabiashara na wavuvi eneo hilo imechangia taka zaidi kuingia ziwani, ikihatarisha afya zao na viumbe majini.

Rai yake, anawaomba wadau wa mazingira, pia mamlaka husika kupambana na kudhibiti hali hiyo, ili kurejesha mialo na maziwa kwa ujumla kubaki salama.

Wadau wa mazingira wanaiambia Nipashe kuhusu wajibu wa kudhibiti plastiki kuchafua Ziwa Victoria na vyanzo vingine vya maji.

Mratibu Mkuu wa Shirika la Synergistic Globe, Angelina Manyama, anaelimu kwa watumiaji na majirani zao, kuhusu haja ya kulinda vyanzo hivyo, ndiyo suala muhimu.

"Elimu hiyo inatakiwa kutolewa kwa watu wote, hususani waliopo karibu na mitaro inayotiririsha maji katika vyanzo vikuu vya maji, vilevile kwa wafanyabiashara na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria, kuhakikisha wanatunza ziwa hilo kwani mifuko ya plastiki inayo sumu," anasema Manyama.

Anasema mara kadhaa, wamekuwa wakitembelea mialo hiyo kwa lengo la kuelimisha, pamoja na kushiriki katika kufanya usafi na kutoa elimu ya utunzaji mazingira, lengo ni kudhibiti shughuli hizo za uchafuzi.

"Kuna haja ya kusimamia kikamilifu sheria za mazingira juu ya wale wanaotumia plastiki, kisha kuzitupa holela hali inayosababisha kuendelea kuonekana kwa uchafu huo katika Ziwa Victoria, vilevile kupitia sheria ya uzalishaji wa plastiki serikali iendelee kuweka mkazo wa kuzuia: anasema.

### BODI ZIWA VICTORIA

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu, anaeleza mikakati ya bodi hiyo kudhibiti uchafuzi ziwani, kupitia shughuli za kibinadamu, anasema jukumu la utunzaji vyanzo vya maji ni la kila mwananchi.

Anaeleza watumishi wa bodi hiyo kwa kushirikiana na watumiaji, pamoja na wanaofanya shughuli zao karibu na vyanzo vya maji, kuhakikisha wanafanya usafi Ziwa Victoria, kwa kuondoa taka ngumu zikiwamo plastiki na magugumaji, huku kuelimishana kukichukua nafasi yake kujihami na athari za uchafuzi wa vyanzo maji.

Kwa mujibu wa Renatus, kosa kisheria kuweka dampo la taka katika eneo lenye chanzo cha maji, hivyo kwa wanaogundulika, wanauchukuliwa hatua za kisheria.

Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria inahimiza uzingatiaji Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009, inaeleza umuhimu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji na kueleza kuwa, palipo na wingi wa watu na uzalishaji taka unakuwa mkubwa.

Pia Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria linataarifu hatua zinazochukuliwa ni kuhakikisha wanadhibiti uchafuzi wa plastiki kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Baraza la Taifa (NEMC) ambao wanawajibika katika kukamata na kufungua mashauri kwa watu wote wanaogundulika kuwa na viwanda vya uzalishaji wa mifuko hiyo, huku wanaotengeneza chupa za plastiki kuhakikisha zinaweza kufanyiwa kazi nyingine na kuweka ufuatiliaji.

### KUTOKA NEMC

Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa, Jarome Kayombo, anaiambia Nipashe, mamlaka yake iko katika hatua kudhibiti uzalishaji bidhaa za plastiki aina zote, isipokuwa zinazotumika kuwa kifungashio kusimamia ubora, mfano hai ni dawa.

Anataja Sheria ya kuzuia Matumizi ya Mifuko ya Plastiki ya Mwaka 2019, inataja makosa matano, ambayo ni: Kuzalisha na kuagiza mifuko ya plastiki; kusafirisha nje; kuhifadhi na kusambaza; kuuza; pia kumiliki na kutumia.

Kuhusu uzalishaji na uagizaji bidhaa za plastiki, au kuziingiza nchini, Kayombo anataja adhabu ni faini kati ya Sh. milioni 20 mpaka Sh. bilioni moja, pia kifungo cha miaka miwili, au vyote kwa pamoja.

Vilevile anasema, kwa wanaotiwa hatiani kusafirisha mifuko hiyo kwenda nje, faini dhidi yao ni shilingi milioni tano hadi Sh. milioni 20, jela miaka miwili, au vyote kwa pamoja.

Aidha, kwa wanaotiwa hatiani kuuza na kusambazaji wa mifuko hiyo katika maeneo mbalimbali nchini, adhabu yao ni kati ya Sh.100, 000 hadi Sh.500, 000, kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Vilevile, sheria hiyo inagusa mtumiaji wa mfuko wa plastiki, adhabu yake ni faini ya Sh.30, 000 hadi Sh.200, 000, kifungo cha siku saba au vyote kwa pamoja.

Hivyo, anaitoa wito kwa wahusika kuacha kujishughulisha na bidhaa hizo, wabaki wazalendo wa kulinda na kutunza mazingira dhidi ya taka za plastiki, inayochangia kulinda viumbe hai.

Mwaka huu, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, mwaka huu yamefanyika kitaifa mkoani Dodoma, yakiwa na kaulimbiu ya 'Pinga Uchafuzi wa Mazingira unaotokana na Taka za Plastiki'.

> **"Vilevile, sheria hiyo inagusa mtumiaji wa mfuko wa plastiki, adhabu yake ni faini ya Sh.30, 000 hadi Sh.200, 000, kifungo cha siku saba au vyote kwa pamoja.**

MAZINGIRA

# Waziri Makamba: Hii hapa mikakati rasmi kupata umeme wa jotoardhi

## • Megawati 9,299 zinazogawanyika kitaifa

**Na Elizabeth Zaya**

MSIMAMO wa serikali hadi sasa, imeamua kuwa na vyanzo vya kuzalisha umeme, ili kuhakikisha inakuwa na nishati inayojitosheleza.

Pia, inaendelea kuvitumia kuzalisha nishati hiyo, ikifanya jitihada za kuongeza vingine, zikiwamo nishati za jua, upepo na jotoardhi.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, akizungunza kwenye Maonyesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika katika viwanja vya bunge jijini Dodoma hivi karibuni, anasema katika kuhakikisha upatikanaji umeme wa uhakika nchini, nguvu kubwa inatarajiwa kuwekezwa kutafuta vyanzo vya jotoardhi.

"Tunachokifanya sasa hivi ni kuongeza vyanzo vingine na kupunguza utegemezi wa maji, ili kwanza kuondokana na 'risk' zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, pia kuwa wa gridi ambayo ni imara zaidi," anasema Waziri Makamba.

"Sisi tumebahatika kuwa na rasilimali za asili nyingi za kuzalisha umeme na tutazitumia zote, nia ni kwamba ikitokea chanzo kimoja kimepata shida, kingine kinaendelea," anasema.

**MTAALAMU JOTOARDHI**

Katika hilo pia kwenye maonyesho hapo, mtaalamu wa Jikokemikali, Ariph Kimani kutoka Kampuni ya Uendelezaji Nishati ya Jotoardhi Tanzania (TGDC), ambayo ni kampuni tanzu ya ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco).

Anataja mikakati yake ni kuongeza vyanzo vingine vya nishati, kwamba tayari wataanza kuchoronga visima vya majaribio ya kuzalisha nishati jotoardhi, katika eneo la Ngozi Mbeya, mashine zake tayari zimeshawasili kutoka China.



Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, akiwa amevaa kifaa maalumu kwenye maonyesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika hivi karibu kwenye viwanja vya bunge jijini Dodoma. Anayemtazama, ni Waziri wa Nishati, January Makamba. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

"Mashine ya Sh. bilioni 13 imeshanunuliwa na imefika nchini tangu Aprili Mosi mwaka huu na Juni mwaka huu, tutaanza kuchonga visima vya majaribio na mradi huo ukimalizika, tunatarajia kuzalisha megawati 70 za umeme. Lengo ni kuzalisha megawati 200, ifikapo mwaka 2025," anasema Kimani.

Anasema, nishati ya jotoardhi inatokana na joto linalotoka kwenye mwamba wenye joto unaochemsha maji yaliyoingia ardhini, akiisifu ni nishati safi, endelevu, akiitaja pia ni rasilimali inayojulikana kuwa jadidifu. Kimani anasema, kutokana na mfumo wa kutumika tena unaorudisha maji ardhini, baada ya mvuke kugeuzwa kuwa maji na kupoozwa, akifafanua ni desturi ya joto linalotoka chini ya ardhi, kwamba kawaida halina kikomo.

Anaeleza kwamba, nishati ya jotoardhi inaanzia kwenye ardhi isiyo na kina kirefu, hadi kwenye maji ya moto na miamba ya joto iliyoko kilomita chache chini ya ardhi, kwenye miamba iliyoyeuka na joto kali inayoitwa kitaalamu 'magma'.

"Wakati dunia inaumbwa ilitokana na miamba ya moto, sasa mwamba unapopoa, unapoteza joto ambalo linaenda kwenye maji, yanapochemka yanakuwa na presha kubwa kiasi kwamba kule ni lazima yatoke, yanachemka huko na yanapotoka yanasafiri yanakuja mpaka kwenye uso wa dunia," anasema Kimani.

Anafafanua, wazo la kuwa na nishati ya jotoardhi, lilianza mwaka 2013, lakini uamuzi ukafanyika mwaka uliofuata 2014, hivyo TGDC ikaanza kazi Desemba ya mwaka 2013, ikibeba jukumu la kuongoza maendeleo ya jotoardhi nchini, ikiwa kampuni tanzu na inamilikiwa na serikali kwa asilimia 100.

Kimani anasema, ikaanza kazi Julai mwaka 2014 kwa jukumu na mamlaka ya kutafiti, kuchimba na kutumia rasilimali za jotoardhi kuzalisha umeme na matumizi mengine ya moja kwa moja.

Anasema TGDC imeanzishwa kwa sababu muda mrefu Tanzania, imekabiliwa na upungufu wa uzalishaji umeme wa kutosha, hata serikali ikachukua hatua za kutatua tatizo la mgao wa umeme, baadhi zikiwa zimeathiri mazingira.

"Kama nilivyosema kwamba, nishati hii inapatikana eneo la bonde la ufa. Tulichofanya cha kwanza, ni kufanya tafiti za kupata maeneo hayo na kisha kutoa kipaumbele kwa baadhi kuanza kuchorongwa visima," anasema.

Kwa mujibu wa Kimani, hadi sasa Tanzania ina rasilimali nyingi za jotoardhi ambazo hazijaendelezwa na kiwango kidogo ndicho kimefanyiwa utafiti, kulingana na makadirio yaliyopo kinadharia.

"Tanzania imejaliwa kuwa na zaidi ya megawati 5,000 za nishati ya jotoardhi zinazosubiri kuendelezwa na chini ya ardhi, kunatarajiwa kubaki joto zaidi kwa mabilioni ya miaka ijayo, hivyo kuhakikisha upatikanaji wa mtiririko wa joto usio na kikomo.

"Mitambo ya umeme ya jotoardhi huzungushwa na mvuke unaotoka ardhini, hivyo kuzalisha nishati ya umeme," anaeleza mtaalamu Kimani.

**MATUMIZI JOTOARDHI**

Anafafanua kuwa matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi ni maji ya moto yatokayo ardhini, yanayoweza kutumika kupasha joto majengo, jengo moja au mji mzima kuchemsha maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani, kuotesha mimea kwenye nyumba za vioo, kukausha mazao, kupasha joto maji kwenye mabwawa ya kufugia samaki na kuua bakteria kwenye maziwa.

"Lengo mahsusi la TGDC ni kuzalisha umeme kutoka katika kisima cha jotoardhi eneo la Ziwa Ngozi, ikiwa ni mwaka wa tano tangu kuanzishwa kwake," anasema na kufafanua:

"Tunawakaribisha wadau mbalimbali kushirikiana bega kwa bega katika kujenga uwezo na kugharamia awamu ya utafiti ya miradi ya jotoardhi na kuendeleza visima vya mvuke nchini Tanzania."

Anasema, manufaa ya nishati ya jotoardhi ni asilia, gharama nafuu na jadidifu na inapatikana kwa uhakika mkubwa zaidi wa asilimia 98, ikizalisha umeme wa uhakika.

Kiamani anataja manufaa mengine, inapunguza athari mbaya za mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa, pia tabianchi, ikitoa nishati safi na salama kwa kutumia sehemyu ndogo ta ardhi.

Pia, Kimani anaisifu kuwa teknolojia iliyothibitishwa na inazidi kuimarika, hata inaweza ikapanuliwa kukidhi mahitaji kwenye eneo dogo kuzalisha umeme, huku ikipunguza moshi zinazochafua mazingira.

Hadi sasa anataja maeneo yaliyolengwa kufanyiwa utafiti huo wa jotoardhi kuwa ni penye ZiwaNatron, Manyara, pia Ngorongoro (Megawati 1000).

Vilevile, Kimani anataja maeneo ya Nyanda za Juu Kusini; Ngozi, Songwe, Mampulo, Kilambo na Kasumulo (Megawati 800); Pwani ya Kusini Mashariki

Luhoi na Utete (Megawati 600); mkoani Morogoro kuna Kisaki, Mtende na Tagalala (Megawati 600); pia mkoani Mara ni eneo la Maji Moto (Megawati 500).

Kwingine anapataja ni; Dodoma kuna Takwa na Mpondi; wakati Singida zipo maeneo ya Hika na Msule; mkoani Shinyanga kuna eneo la Ibadakuli (Megawati 500); Kagera ipo Mtagata, Amboni Tanga, Maji Moto, Katavi, Rock Of Hades, Rukwa, Ushirimbo- Geita, pia Kigoma na Iringa, jumla yao kunatarajiwa kuwapo megawati 1000.

Anasema umeme wa jotoardhi kwa upande wa Afrika, nchini Kenya ndiko kunakoongoza kwa kuzalisha megawati 1000, ikifuatiwa na Ethiopia inayozalisha megawati 7.2 na kimataifa, Marekani inaongoza kuzalisha zaidi ya megawati 3200.

# VITA MAZINGIRA VYA RAIS, MCHANGANUO WAKE UNAVYOJITOKEZA KWENYE BAJETI

**Inatoka Uk. 11**

wakati na kuharibikia njiani, hali inayopelekea kutupwa na kusababisha athari za kimazingira, ikiwamo kuongeza uchafu na kuzalisha gesi inayokwenda kuziba 'ozone layer' (anga)" anasema Sara.

Vilevile anahimza pesa za bajeti zitumike kumsaidia mkulima kwa kilimo cha kisasa na matumizi bora ya mazuri ya ardhi, ili kuleta uhimilivu wa ardhi kwenye mabadiliko ya tabianchi.

Sara anapendekeza kuwapo utafiti wa athari za kimazingira kama vile maeneo ardhi oevu, wanyama walio hatarini kupotea na kuwapo taarifa sahihi za maendeleo ya mazingira, ili kuzisaidia serikali, taasisi binafsi na wadau wa mazingira wapate uhalisia na kwa wakati sahihi, kuwaongoza vyema kwenye mapambano ya mazingira kitaifa.

Anashauri fedha kufikia maeneo kama ya elimu kwa jamii vijijini, kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake, ili wajue nafasi yao katika kukabiliana na hali hiyo inayokwamisha serikali katika vita vyake.

"Vilevile pesa hizi wangegawiwa kitengo cha majanga nchini, ili kuwasaidia wananchi wanaoathiriwa na majanga yatokananyo na mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko, mmomonyoko wa udongo," anafafanua.

Mkurugenzi wa Tanzania Cleanup and Conservation Initiatives (TCCI), Salum Kigungo, anashauri busara ya pesa za bajeti kuelekezwa, pia kwenye miradi ya nishati mdalala ya kupikia ikiwamo makaa ya mawe, na unaotengenezwa kwa taka na gesi.

Anasistiza mkakati wa kufikiwa vita vya kukabili taka za plastiki mitaani na kuanzishwa viwanda vya mbolea kama vike mboji kwa taka za aina hiyo, zinazkiongoza kuzagaa mitaani.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mikakati ya Maendeleo Endelevu (TSDI), Fredy Kwezi, anapongeza uamuzi wa serikali kuongeza kodi kwenye magari yaliyotengenezwa muda mrefu, kuwa yatadhibiti taka zinazotokana na magari chakavu.

Fredy anasema, pia kupandishwa kodi kutapunguza uingizwaji bidgaa hiyo nchini, hata kudhibiti uzagaaji taka zake mitaani.

" Serikali yetu inapambana sana, sasa ni wakati wa wananchi kuiunga mkono kwa vitendo na hapa naongelea kubadili mtindo wa maisha ikiwezekana tutumie zile za zamani za vitambaa, ambazo hudumu muda mrefu," anaeleza.



## HABARI DODOMA

# ‘Watanzania acheni kuiga mila, desturi za wazungu’

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Fadhil Maganya, amewataka Watanzania kuacha tabia ya kuiga mila na desturi za mataifa ya nje kupitia mitandao na teknolojia ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili ambao umeanza kushika kasi katika jamii.

Akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti katika ziara yake kwenye Wilaya ya Iramba, Manyoni, Ikungi, Mkalama, Singida DC na Manispaa ya Singida mkoani hapa kukagua miradi ya maendeleo, Maganya alisema kumekuwa na mmomonyoko wa maadili katika jamii kutokana matumizi ya mitandao na teknolojia.

“Sasa hivi utakuta mtu yupo hapa Iramba lakini anaangalia vitu vilivyopo Marekani kwa kupitia mtandao, tusipokuwa makini na matumizi ya hii mitandao tutajikuta tunaacha mila na desturi zetu,” alisema.

Alisema kuwa vijana wengi ndiyo wapo katika changamoto ya mmomonyoko wa maadili na endapo wazazi na walezi hawatakuwa imara kusimamia malezi ya watoto wao taifa litakuwa na vijana wasio na maadili.

Maganya aliwataka viongozi wa chama na serikali kuhakikisha wanasimamia miradi inayotekelezwa kwenye halmashauri ili ijengwa kwa viwango na ubora unaotakiwa kwani serikali inatoa fedha nyingi kutekeleza miradi hiyo.

Hata hivyo, akiwa katika ziara hiyo wananchi wa kijiji cha Ishenga walishukuru serikali kwa kujenga shule mpya ya Nkindiko itakayosaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Ishenga.

Naye Mkazi wa Kijiji cha Ishenga, Jumanne Mpondo, alisema katika Shule ya Msingi Ishenga, darasa moja lina kuwa na zaidi ya wanafunzi 200, hali ambayo inasababisha walimu kushindwa kufundisha kwa ufanisi.

# Ziara ya Chongolo yala ‘kichwa’ Meneja RUWASA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZIARA ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, Mkoa wa Dodoma imemwondoa kwenye wadhifa Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) wa mkoa huo, Mhandisi Godfrey Mbabaye, kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM mkoani humo, wananchi wa majimbo mbalimbali walikuwa wakilalamikia kero ya maji licha ya serikali kutoa fedha ya utekelezaji wa miradi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alichukua hatua hiyo kwa mamlaka aliyonayo kupitia Sheria Namba Tano ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.

**Niwahakikishie, nimeyaona, nimeyachukua mwenyewe naenda kumwambia aliyewateua kuhusu mambo yanavyoendelea na namna ambavyo sijaridhika na utatuzi wa changamoto ya maji.**

Aweso alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, kuunda timu ya wataalamu ya kufuatilia kero za utekelezaji wa mradi wa maji mkoani humo na kutoa suluhisho la kumaliza tatizo hilo mara moja.

Aidha, aliitaka timu hiyo na katibu huyo ifanye tathmini ya utendaji kazi wa mameneja wa wilaya zote wa RUWASA.

Chongolo akiwa katika ziara ya kichama wilayani Chemba, Mbunge wa jimbo hilo, Mohamed Moni alimweleza kuwa hakuna mradi wa maji ambao umeanzishwa wilayani hapo na kukamilika zaidi ya maneno matupu.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mrijo Chini, Chongolo alisisitiza kuwa hajaridhishwa kabisa na miradi ya maji katika wilaya nzima ya Chemba.

Alisema hajaridhishwa na usimamizi wa miradi ya maji ambayo imechangia vijiji vingi vya wilaya hiyo kukosa maji licha ya miradi kuanzishwa lakini utekelezaji wake ni hasi.

“Niwahakikishie, nimeyaona, nimeyachukua mwenyewe naenda kumwambia aliyewateua kuhusu mambo yanavyoendelea na namna ambavyo sijaridhika na utatuzi wa changamoto ya maji, nimezunguka maeneo yote sijaridhishwa kabisa,” alisema Chongolo.

Aliongeza: “Hatuwezi kukaa tukabembelezana kwa mambo ya msingi wakati wananchi mnataka matokeo na sisi tuliahidi kuyatatua sasa kama mtu hataki kuyafanyia kazi aende akalime kwao asikae kwenye nafasi ya kushughulikia matatizo ya wananchi.”

Juni 15, 2023 akiwa Wilaya ya Mpwapwa alimtaka Aweso kufika huko kutatua tatizo la maji Kijiji cha Lupeta na siku iliyofuata aliitwa tena Kijiji cha Pwaga wilayani humo.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, akizungumza na maofisa habari wa wizara pamoja taasisi kutoka Zanzibar katika kikao kilichofanyika mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Dk. Yonazi awafunda maofisa habari serikalini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi amewataka maofisa habari serikalini kuendelea kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku badala ya kufanya kwa mazoea.

Dk. Yonazi alitoa rai hiyo baada ya kutembelewa na maofisa habari hao kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ofisini kwake kwa lengo la kuangalia na kujifunza utendaji kazi wa vitengo vya habari, mawasiliano na uhusiano kwa Tanzania Bara.

Alisema ipo haja ya maofisa habari kubadili mitazamo katika kuhabarisha umma kwa kuangalia mabadiliko ya kiteknolojia kwa kutumia mifumo ya kisasa inayoendana na wakati uliopo.

“Hivyo kuna umuhimu kuwa wabunifu katika kuibua habari na siyo kusubiri matukio ya viongozi ndipo mhabarishe umma, hakikisheni teknolojia haiwaachi nyuma bali mnaendana nayo katika kupashana habari,” alisema.

Alisema pamoja na kuhabarisha ni muhimu kuandika habari zinazozingatia maadili na taaluma ili kuwa na habari zinazoishi na kuufaa umma.

Aidha, aliwakumbusha maofisa hao kujali muda katika kutoa taarifa na vyanzo vya kuaminika ili kuepuka makosa yanayojitokeza endapo mambo hayo hayatazingatia.

“Lazima matukio na habari zitolewe kwa wakati na zenye ubora huku mkizingatia aina ya walaji wa habari hizo na kutumia njia sahihi za usambazaji wake,” alisisitiza Dk. Yonazi.

Hivyo, aliwahimiza maofisa hao kujifunza lugha zaidi ya moja ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya kuhabarisha umma kwani wanawafikiwa watu wengi ikiwamo wa mataifa mengine.

# Uhaba nyumba za walimu wafikia 255,097



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hadi hadi Mei, 2023 kuna upungufu wa nyumba za walimu 255,097 huku zilizopo vijijini ni 55,097.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni nyumba ngapi zinahitajika kwa watumishi wa umma waliopo vijijini.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema kwa upande wa watumishi wa afya, nyumba za watumishi zilizopo ni 7,818 na upungufu ni nyumba 15,272.

Aidha, alisema katika kukabiliana na upungufu wa nyumba za watumishi wa kada za ualimu na afya hususani waliopo vijijini, serikali inakamilisha mchakato wa kujenga nyumba 212 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni mwaka huu kupitia mradi wa SEQUIP.

Pia, Ndejembi alikiri kuwa kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za watumishi waliopo vijijini hususani watumishi wa kada za elimu na afya.





# Wafugaji, wafanyabiashara walia ukosefu wa viwanda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFUGAJI na wafanyabiashara wa mazao ya mifugo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wamelalamikia ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao hayo hali inayosababisha kukosa fursa ya masoko na nje ambayo yana tija zaidi kuliko ya ndani.

Wadau hao wamedai kuwa mikoa hiyo ni miongoni mwa maeneo nchini yenye mifugo mingi lakini haina tija nzuri kutokana na kukosekana kwa viwanda hivyo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti waliomba serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kujenga viwanda ama kualika wawekezaji kutoka nje wanaoweza kuwekeza kwenye viwanda hivyo ili kuwasogezea soko.

Mmoja wa wadau hao, Aloyce Shija ambaye ni mfugaji na mfanyabiashara wa mifugo, alisema wamekuwa wakizalisha ngozi na mazao mengine ya mifugo lakini mengi yanatupwa kwa sababu hakuna viwanda vya kuyaongeza thamani.

Alisema hali hiyo inawafanya kupata faida kubwa kama ilivyo kwenye mazao mengine yakiwamo ya kilimo kwa maelezo kuwa sehemu kubwa ya mazao hutupwa.

**Sasa kama kungekuwapo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo Uwanja wa Ndege Songwe ingekuwa ni fursa kubwa kwa wananchi, uwekezaji ni mkubwa lakini bidhaa za kusafirisha hakuna na wanufaika wakubwa ni wageni.**

"Ukiangalia katika maeneo mengi ya mikoa hii, mifugo ni mingi sana, ukienda maeneo kama Chunya, Mbarali, Momba, Sumbawanga na Songwe huko kuna mifugo mingi lakini tunachouza ni nyama na maziwa, lakini kuna mazao mengine soko halipo," alisema Shija.

Alisema katika mataifa mengine mifugo ikichinjwa yapo mazao yanahitajika viwandani kama kwato, pembe na ngozi ambayo yanahitajika viwandani kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zingine.

Alisema asilimia kubwa ya mazao hayo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yanatupwa kwa sababu havipo viwanda vya kuyachakata ili yapelekwe kwenye masoko.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali inapoteza mapato ambayo yangepatikana kutokana na usafirishaji wa mazao hayo ya mifugo kupitia masoko mbalimbali.

Mfanyabiashara wa ng'ombe katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo, Joel Amos alisema kutokana na mahitaji makubwa ya nyama nje ya nchi serikali inapaswa kutengeneza fursa ambazo zitasaidia uchakataji wa mazao hayo.

Alisema katika mikoa hiyo kuna kila aina ya njia za usafirishaji ambazo zingetumika kusafirisha mazao hayo ukiwamo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

"Sasa kama kungekuwapo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo Uwanja wa Ndege Songwe ingekuwa ni fursa kubwa kwa wananchi, uwekezaji ni mkubwa lakini bidhaa za kusafirisha hakuna na wanufaika wakubwa ni wageni, " alisema Amos.

Ofisa Mifugo kutoka katika Bodi ya Nyama Tanzania (TBM) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Mpoki Alinanuswe, alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kwamba kwa kanda hiyo kuna kiwanda kimoja pekee.

Alisema kwa sasa kanda hiyo wafugaji wamekuwa wakifuga kisasa na kuzingatia kanuni za ufugaji kibiashara lakini tatizo ni namna ya kuyafikia masoko ya nje ya nchi.

Alisema kupitia sekta ya mifugo wamekuwa wakihamasisha ufugaji wa kibiashara na kuongeza thamani ya ng'ombe sambamba na utunzaji wa chakula cha kutosha katika msimu wa mavuno ya mazao ili wauze kwa bei nzuri.




Askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mbeya wakiwa wamemaliza kuuzima moto uliokuwa unaanza kuwaka kwenye moja ya malori ya kubebea mafuta jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watumishi wapya wapewa zigo la kuinua ufaulu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa idara ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wametakiwa kuutumia vizuri muda wanaotakiwa kuwapo kwenye vituo vyao vya kazi ili kuinua kiwango cha ufaulu katika ngazi mbalimbali za elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Stephen Katemba, aliyasema hayo alipofanya kikao na walimu waliojiriwa hivi karibuni ambao wameanza kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi.

Alisema walimu hao wanatakiwa wahakikishe wanayatumia maarifa waliyoyapata kwenye vyuo mbalimbali kuhakikisha wanawafundisha vizuri wanafunzi na kuhakikisha wanafikia malengo wanayokuwa wamewekewa.

Alisema serikali imewaandaa vizuri walimu hao na inatarajia kupata matokeo chanya kwenye vituo vyao vya kazi ambavyo wamepangiwa hasa kwa kuhakikisha wanawafundisha vizuri watoto.

"Kwenye utumishi ni lazima utumie vizuri rasilimali za umma, lakini hata muda ni rasilimali muhimu ambayo mnatakiwa kuitumia vizuri, mnatakiwa mfike kazini saa 1:30 asubuhi na kutoka saa 9:30 alasiri," alisema Katemba.

Alisema wanapotoka kazini wanatakiwa kuhakikisha wametimiza majukumu yao ipasavyo hasa kuhakikisha wamefundisha vipengele vyote wanavyotakiwa kufundisha.

## Ileje yajipanga kuzalisha pareto tani 3,000

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

SERIKALI wilayani Ileje katika Mkoa wa Songwe, imeweka mikakati ya kuongeza kiwango cha uzalishaji wa pareto kutoka wastani wa tani 1,000 mpaka 3,000 kwa mwaka katika msimu ujao wa kilimo kwa kuanza kuwajengea uwezo wakulima.

Wakulima wa zao hilo katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo wameanza kupatiwa mafunzo maalumu ya kuongeza uzalishaji kwa kulima kisasa na kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti na wataalamu wa zao hilo.

Aidha, serikali imeanza kuhamasisha wakulima kuunda vikundi ili walime mashamba makubwa ya zao hilo ambayo yatakuwa na tija kuliko ilivyo sasa ambapo kila mkulima anazalisha kivyake.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Farida Mgomi aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kuhamasisha wakulima wa pareto katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Alisema kwa sasa wilaya hiyo inashika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa pareto baada ya Wilaya ya Mbeya ambayo ndiyo inaongoza kitaifa na kwamba wanafanya juhudi za kuhakikisha uzalishaji unaongezeka mara dufu.

"Kwa kushirikiana na maofisa kilimo wilaya tutahakikisha msimu ujao wa kilimo uzalishaji unaongezeka mpaka tani 3,000, tunaamini kwamba tukifikia kiwango hicho hata wakulima wetu watapata tija zaidi na hata halmashauri itapata mapato," alisema Farida.

Alisema kwa sasa pareto inayozalishwa wilayani humo inauzwa katika Kampuni ya Pyrethrum Company Limited (PCT) yenye kiwanda cha kuchakata zao hilo katika Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa ambayo mahitaji yake ni tani 6,000 kwa mwaka.

Alisema wilaya hiyo ilituma wataalamu kwenda kupata mafunzo katika kiwanda hicho kwa lengo la kuwaongezea ujuzi watakaoutumia kuwahamasisha wakulima.

Mgomi alisema uwepo wa soko hilo utapaisha bei ya pareto kutoka Sh. 3,500 ya sasa kwa kilo moja mpaka Sh. 4,200 na hivyo kuwaongezea tija wakulima.

Ofisa Kilimo Wilaya, Herman Njeje alisema ili kufikia malengo wataunda vikundi vya wakulima ambavyo vitapatiwa elimu ya kilimo bora cha pareto kwa kuwafuata katika maeneo yao ili waongeze uzalishaji na kupata tija zaidi.

Alisema wakulima kwa vikundi itakuwa rahisi zaidi kwa

# Ujenzi kilomita 103 za barabara kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, Jamal Kassim Ali, amesema kujengwa kilomita 103 za barabara na Uwanja wa Ndege wa Pemba kutasaidia kukuza uchumi na kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 103 Unguja na Pemba.

Alisema kwamba ujenzi wa miradi hiyo unatekelezwa kupitia fedha za mkopo Sh. trilioni 1.4 kutoka Taasisi ya Fedha ya Uingereza (UKEF's) kupitia Benki ya Citi na Benki ya Deutsche.

"Mpango wa kukopa fedha tuliuanza mwaka 2020 baada ya Serikali ya Awamu ya Nane kuingia madarakani na huu utakua ni mradi mkubwa kwa Zanzibar na haujawahi kutokea," alisema Jamal ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

"Sekta ya miundombinu inagusa maeneo yote ya kiuchumi ikiwamo sekta ya utalii, wakulima, wavuvi, wafugaji wote wanategemea miundombinu ya barabara," alisema.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema mradi huo utahusisha Barabara ya Fumba/Kisauni kilomita 12, Tunguu/ Makunduchi kilomita 48 kwa Unguja na kwa Pemba Mkoani/Chakechake kilomita 43.

Aidha, alisema Uwanja wa Ndege wa Pemba ulijengwa mwaka 1973 na sasa umepitwa na wakati ndiyo maana serikali imeamua kujenga uwanja wa kimataifa hatua ambayo itasaidia kuimarisha sekta ya utalii na huduma za kijamii kwa wananchi.

"Mradi huu ni wa kihistoria kwa Zanzibar na haujawahi kutokea tangu kufanyika mapinduzi mwaka 1964 kujenga barabara zenye urefu huo kwa wakati mmoja hii ni hatua kubwa ya maendeleo," alisema Dk. Khalid.

Hata hivyo alisema mradi huo pia ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Dk. Mwinyi aliyoitoa wakati wa kampeni kuwa atajenga uwanja wa kisasa Pemba na kuimarisha miundombinu ya barabara.

Balozi wa Uingereza, Devid Concar, alisema kwamba miradi hiyo ina umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar katika kukuza uchumi na huduma za jamii kwa wananchi.

"Serikali ya Uingereza inamatumaini fedha za mradi huo zitawanufaisha Wazanzibari katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii na Serikali ya Uingereza itaendelea kuunga mkono Zanzibar katika kuharakisha maendeleo kwa wananchi wake," alisema.

Aidha, alisema ana matumaini makubwa na kampuni zilizopewa kazi za ujenzi huo ikiwemo Kampuni ya Mecco na kampuni ya Propav zitatekeleza mradi huo kama walivyokubaliana kabla ya kufikiwa kwa mkataba huo.

Mwakilishi wa Tunguu ambaye ni Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhamed Said, alisema miradi hiyo ina umuhimu mkubwa katika kukuza sekta ya utalii Zanzibar na kufikisha huduma za uhakika za miundombinu kwa wananchi.

"Sekta ya utalii ni nguzo ya uchumi wa Zanzibar na kuimarika kwa miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege kutasaidia kukuza zaidi sekta ya utalii na huduma za kijamii kwa wananchi," alisema Simai.

Mkataba huo umesainiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ofisi za Zanzibar zilizopo Kinazini.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum (katikati), akitia saini hati ya makubaliano ya mkopo wa Sh. trilioni 1.4 kutoka Taasisi ya Fedha ya Uingereza (UKEF's) kupitia Citi Bank na Deutsche Bank zitakazotumika katika miradi ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba, barabara ya Tunguu/ Makunduchi, Fumba / Kisauni na Mkoani/Chakechake. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Citi Bank, Geoffrey Mchangila na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yafafanua matumizi ya mtaala mmoja wa elimu Bara, Visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema masuala ya elimu ya sekondari hayapo katika mambo ya muungano.

Imesema lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ni bora kutumia mtaala mmoja wa ngazi ya elimu hiyo kwa ajili ya kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu suala la Zanzibar kutumia mitaala ya masomo ya sekondari ambayo siyo mambo yaliomo katika orodha ya muungano.

Alisema kuwapo kwa mtaala wa masomo ya sekondari kwa kiasi kikubwa yamewajengea uwezo wanafunzi kutoka Zanzibar kuingia katika ushindani wa masomo na wenzao kutoka Tanzania Bara.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya kikosi kazi katika kupitia mfumo wa elimu wa Zanzibar, imetoa mapendekezo yake ikiwamo kupitiwa kwa muundo wa elimu ya Zanzibar ambayo itakwenda sambamba na mageuzi yaliopo sasa.

Alisema kwa sasa katika muundo wa elimu uliopo sasa suala la elimu ya juu ya sekondari ni mambo ya muungano ambapo wanafunzi kutoka Zanzibar wanafanya mtihani unaosimamiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) ambayo ni taasisi ya muungano.

Hata hivyo alisema utafiti uliofanywa umebaini kwamba wanafunzi kutoka Zanzibar ambao wanafanya mitihani ya taifa ya sekondari na wenzao kutoka Tanzania Bara wanafanya vizuri na kufaulu kuingia vyuo vikuu.

Alisema: "Mheshimiwa Spika matokeo yanatuonesha kwamba wanafunzi kutoka Zanzibar wanafanya vizuri na kufaulu katika mitihani ya taifa kama wenzao wa Tanzania Bara."

# TAMWA-ZANZIBAR yazindua mwongozo wa sera jinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-ZANZIBAR) imezindua mwongozo wa sera ya jinsia kwa vyombo vya habari utakaozingatia malengo ya kijinsia na kufikia malengo ya nchi na kidunia.

Hafla ya uzinduzi huo ilifanyika jana katika ofisi za chama hicho zilizopo eneo la Tunguu Zanzibar, kuwashirikisha baadhi ya wamiliki wa vyombo vya habari, waandishi wa habari na watendaji wa serikali.

Mkurugenzi wa chama hicho Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema masuala ya kijinsia yanatiliwa mkazo duniani, hivyo vyombo vya habari kama mdau wa kuimarisha usawa wa kijinsia ni vyema kuwa na sera na mikakati ya kutekeleza ili kutoa mchango wake.

"Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu muhimu ikiwamo dawati la kijinsia katika vyombo vya habari, unyanyasaji wa kingono, chimbuko la mwongozo huo na malengo yake," alisema Dk. Mzuri.

Alisema pamoja na jitihada za kuleta usawa wa kijinsia lakini bado hakuna usawa wa kijinsia hasa katika masuala ya uongozi, uchumii na kijamii.

Alisema kwenye uongozi utafiti duniani zinaonyesha kwamba wanawake katika uongozi ni chini ya asilimia 30 na kwa Afrika Rwanda ndiyo inayoongoza kwa wanawake kuwa na nafasi nyingi.

Alisema utafiti unaonyesha pia habari za wanawake hazipati nafasi nzuri katika vyombo vya habari kutokana na mifumo dume na kwa miaka mingi wanawake huachwa nyuma na kutotumia fursa kwa vyombo vya habari.

Dk. Mzuri alisema baadhi ya wahusika katika vyombo vya habari wanajihusisha na rushwa za ngono ambayo huathiri zaidi wanawake hasa vijana na uwakilishi mdogo wa vyombo vya maamuzi.

Hata hivyo alisema vyombo vya habari vinapaswa kusimama imara kutekeleza masuala ya jinsia ili wanawake na wanaume kufaidika katika kupata haki na fursa zilizopo nchini.

Baadhi ya washiriki katika hafla hiyo waliipongeza TAMWA kwa kutoa mwongozo huo wa sera, wakisema ni vyema vyombo vya habari kuwa na sera ya jinsia na dawati la jinsia ili kuhakikisha wanawake wanapata haki zao stahiki.

Imane Duwe, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alisema kuna changamoto nyingi katika vyombo vya habari ambazo wanakumbana nazo wanawake ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa Dar Es Salaam**
**Usimamizi wa mirathi Na.900 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HAFSA CHARLES LUPEMBE WA KIPUNGUNI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA FARIDA CHARLES LUPEMBE**
**HEMEDI NASSORO PELEMBA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 mwezi 7 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 19 mwezi 06 mwaka 2023

## KUPOTEA KWA CHETI



**GONZAGA RWEHUMBIZA RUGAMBWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0534-0125** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. ANTHONY'S SECONDARY SCHOOL MBAGALA** mwaka 1998. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chocote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/210467/2023**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JENIFA SALVATORY KISHE** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 581 CPF** aina ya Guta. Chassis namba King Lion **200100034.** Engine namba **KL163ML220010034.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/URA/RB/210880/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA.180 YA MWAKA 2023**
**MICHAEL MAKOYE KISUSI......................... MDAI**
**VERSUS**
**IBRAHIM ISAYA CHIHUYO......................... MDAIWA**

**KWA: IBRAHIM ISAYA CHIHUYO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayomaelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe **06.07.2023 saa 3.00 asubuhi.** Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO: -** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **09 ya Mwezi wa JUNI,2023**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 77 YA 2023**

**ALICE MWAIPOPO KAVEMBA...........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**LUSEGA ELIAS MWACHINYEMBA**
**SALUM MBEGA**
**MOHAMED SAID ALMASI ..........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**SALUM MBEGA** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe **13/7/2023** mbele ya Mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe **19, mwezi Juni, 2023**

M.Khasim
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT-SUB REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.219 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CHRISTOPHER BARNABAS MZOO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**STEVEN BARNABAS MZOO**
**NOTICE TO CREDITORS**
**(Rule 111)**

Notice is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named CHRISTOPHER BARNABAS MZOO deceased, who died at Mikocheni Dar es Salaam on 13th day of October 2018 and whose latter of administration was granted on 22 day of March 2023 to me by the Court.
All creditors are hereby required to send in their claims to me at the following address within 60 days (two months) from the date of publication of this Notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regards only to the claims of which I shall then have had notice.

STEVEN BARNABAS MZOO
(Administrator)

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PAMELA WILFRED KIIZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 622 CWX** aina ya **TVS - 125.** Chassis namba **MD625AF45M1C10082.** Engine namba **DF4CM1X09884.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/170323/2023.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

### KUANZA KWA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2023/2024

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza.

**NFRA** hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Kwa mzimu huu wa mavuno ununuzi utaanza rasmi tarehe tarehe 22 Juni, 2023.

**Mazao na Malengo ya Ununuzi:**
- Mahindi tani 200,000
- Mpunga tani 200,000

**Njia za Ununuzi Zitakazotumika:**
- Kutumia vituo vya ununuzi-Muuzaji yeyote anaweza kupeleka nafaka zake kuuza;
- Vikundi vya Wakulima/Ushirika-Vitaingia makubaliano maalum na NFRA;
- Mawakala/wafanyabiashara wa mazao - Wataingia makubaliano maalum na NFRA.

**Vituo vya Ununuzi:**
Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa wa Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa wa Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Manyoni), Arusha (Arusha na Manyara) na Shinyanga (Mkoa wa Kigoma na Tabora). Aidha, mpunga utanunuliwa katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya na Tabora.

**Utaratibu wa Ununuzi:**
Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Bei elekezi zitakazotumika zitapangwa kwa kuzingatia umbali kutoka ghala kuu la NFRA na bei za soko katika eneo husika. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima na Mawakala utafanyika kupitia makubaliano yatakayofikiwa baina ya Kanda ya NFRA na Vyama/Vikundi husika.

**Utaratibu wa Malipo:**
Malipo yote yatafanyika ndani ya siku tatu baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**
**20 Juni, 2023.**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wapigambizi wagundua vishindo utafutaji wa nyambizi ya Titan

**WASHINGTON, Marekani**

MSAKO wa kutafuta nyambizi ndogo iliyopotea katika bahari ya Atlantiki unaendelea kwa kasi, huku waokoaji waliokuwa wakitafuta sehemu ya chini ya maji wakisema wamegundua sauti za kutisha.

Nyambizi hiyo ya kitalii iliyopotea karibu na eneo iliyotokea ajali ya Titanic na kuelezea walisikia sauti za kishindo zikitoka karibu na eneo ambalo nyambizi hiyo ndogo ilipotea.

Kwa mujibu wa taarifa ya ndani ya serikali ya Marekani, iliyoonekana na vyombo vya habari vya Marekani, ilieleza sauti hizo zilisikika kila baada ya muda wa dakika 30 Jumanne.

BBC iliwasiliana na Idara ya Usalama wa Taifa na Walinzi wa Pwani kwa ajili ya kuzungumzia hali hiyo.

Vyombo vya habari vya CNN na Rolling Stone zote ziliripoti juu ya uwepo wa sauti hizo.

Watu watano walikuwa kwenye chombo hicho wakati mawasiliano yalipopotea saa moja na dakika 45, baada ya kuanza safari yake Jumapili.

Kulingana na walinzi wa Pwani ya Marekani, watu hao wana chini ya saa 30 pekee ya kupata hewa ya oksijeni ambayo iliyobakia ndani ya chombo hicho.

Operesheni ya utafutaji katika jimbo la Newfoundland nchini Canada hadi sasa imeshindwa kupata chochote.

Hata hivyo, msako huo umeongezwa kwa upana kwa kujumuisha rasilimali zaidi na utaalamu wa uokoaji kutoka kwa kampuni binafsi.

Mpigambizi, Dik Barton, kutoka Uingereza ambaye ameona ajali ya Titanic, alisema eneo hilo ni hatari sana.

"Kuna mteremko wa ndani na mkondo wa maji ambao huzunguka. Nguvu ya chini ya maji ni ndogo," alikiambia kipindi cha Good Morning Britain cha ITV.

Akizungumzia kuhusu jinsi chombo hicho kingeweza kupatikana, Barton aliongeza kuwa huenda itabidi kurejeshwa ardhini kwa kuwa hakuna njia ya kuipata nyambizi hiyo chini ya bahari.

Hata hivyo, klabu ya wagunduzi, ambao wanajitolea kusaidia kutafuta mahali ambapo nyambizi iliyotoweka, walisema kwa kutumia roboti za chini ya maji kutoka kampuni ya Magellan ya Uingereza imegundua chombo hicho kipo eneo hilo.

Watu wawili waliomo kwenye meli ya chini ya maji, Hamish Harding na Paul-Henri Nargeolet, ni wanachama wa klabu hiyo, mtandao wa kimataifa wa uchunguzi wa kisayansi.

Garriott alibainisha kuwa kumekuwa na dalili za uwepo wa uhai wakati msako huo ulipoingia katika saa yake muhimu baada ya kusikika sauti za kishindo ziliripotiwa hapo awali katika eneo ambalo nyambizi hiyo ipo.

Mtaalamu wa meli ya Titanic Tim Matlin, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba sakafu ya Bahari ya Atlantiki katika eneo ambalo meli ya Titanic imejikita ni nyeusi na ina baridi kali.

Mbali na hayo, sehemu ya bahari kuna matope na yanatiririka kiasi ambacho huwezi kuona mkono wako mbele ya uso wako. Njia pekee ya kupata mahali kilipo chombo hiki ni kwa kitu kinachoitwa sonar, kwani hata rada haifanyi kazi.

Matlin aliongeza: "Kwa hiyo ninahofia maisha ya watalii hao ambao wako kwenye meli yapo hatarini."

**BBC**



Ndugu wa wafungwa wakiomboleza nje ya gereza nchini Honduras baada ya vurugu zilizohusisha magenge hasimu ndani ya jela kusababisha vifo. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Biden aichefua tena China

**CALIFONIA, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amemtaja kiongozi wa China Xi Jin Ping, kuwani dikteta wakati akihutubia hafla ya kuchangisha fedha huko California.

Matamshi yake yanakuja siku moja baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, kukutana na Rais Jin Ping na kufanya mazungumzo mjini Beijing, ambayo yalilenga kupunguza mvutano kati ya mataifa hayo mawili yenye nguvu.

Katika taarifa yao, Rais Jin Ping alisema baadhi ya mafanikio yamepatikana, huku Blinken akidokeza kwamba pande zote mbili ziko tayari kwa mazungumzo zaidi.

Hata hivyo, China bado haijajibu matamshi ya Rais Biden.

Rais Biden, katika hafla ya kuchangisha pesa iliyofanyika juzi usiku, pia alisema Jin Ping alikuwa na aibu juu ya mvutano wa hivi majuzi kuhusu puto la kijasusi ya uchina ambayo ililipuliwa juu ya Marekani.

Ziara ya Blinken mjini Beijing ni ya kwanza kwa mwanadiplomasia mkuu wa Marekani katika takriban miaka mitano.

Ziara hiyo ilianzisha upya mawasiliano ya ngazi ya juu kati ya nchi hizo mbili.

Biden na Jin Ping walipongeza hatua hiyo kama nzuri, licha ya waziri huyo wa Marekani kuweka wazi kuwa tofauti kubwa zimesalia kati ya nchi hizo mbili.

Marekani na China zimekuwa zikipingana kwa muda mrefu kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo biashara, haki za binadamu na Taiwan.

Lakini uhusiano umezorota katika mwaka uliopita.

**BBC**

# Wafungwa 41 wauawa katika ghasia

**TEGUCIGALPA, Honduras**

WATU 41 wameuawa katika ghasia gereza la wanawake nchini Honduras zilizotokea juzi.

Ilifahamika kuwa mapigano yalizuka kati ya magenge hasimu, wakati genge moja liliwasha moto katika jela wanayoishi wafungwa kutoka upande mwingine.

Maofisa walisema moto huo ulisababisha vifo vingi lakini kuna baadhi ya wafungwa waathiriwa walipigwa risasi.

Naibu Waziri wa Usalama wa nchi hiyo, Julissa Villanueva, alitangaza hali ya hatari na kuahidi kukabiliana na ghasia hizo.

Pia aliidhinisha kuingilia kati mara moja kwa wazima moto, polisi na wanajeshi.

"Hasara ya maisha ya binadamu haitavumiliwa," alisema Villanueva alisema.

Haijulikani ikiwa wafungwa wote waliouawa walikuwa wafungwa wa jela hiyo, ambayo iko takriban kilomita 20 kutoka mji mkuu wa Honduras, Tegucigalpa, ambayo ilikuwa na watu 900.

Wafungwa wengine kadhaa wamepelekwa hospitalini baada ya kupata majeraha.

Delma Ordonez, ambaye anawakilisha wanafamilia wa wafungwa, aliviambia vyombo vya habari vya ndani sehemu ya gereza imeharibiwa kabisa katika ghasia hizo.

Video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha wingu kubwa la moshi wa kijivu ukipanda kutoka kwa gereza la wanawake.

**BBC**

**Haijulikani ikiwa wafungwa wote waliouawa walikuwa wafungwa wa jela hiyo, ambayo iko takriban kilomita 20 kutoka mji mkuu wa Honduras, Tegucigalpa, ambayo ilikuwa na watu 900.**

## HABARI MICHEZO

# BRAZUKA, EFM KUVUMBUA VIPAJI

**Na Saada Akida**

TAASISI ya Michezo ya Brazuka kwa kushirikiana na Redio EFM na TV E wameanzisha kampeni ya kusaka vipaji vya soka na kuviibua nchi nzima wakipanga kutembea kwenye wilaya 139.

Katika kampeni hiyo iliyozinduliwa jana jijini Dar es Salaam, wamepanga kuibua vipaji vya vijana 200,000 ambapo malengo yao ni kupata vijana 14,000 kwenye kila wilaya na kuwapa nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Uendesha wa kituo cha EFM na TV E, Dennis Busurwa (Sebbo), alisema lengo la mpango huo ni kuweza kusaidia soka la Tanzania na kuwapa urahisi klabu kubwa na nyingine hapa nchini kuweza kupata wachezaji vijana kwenye timu zao ambao hawaonekani kwa sababu ya kutofikiwa.

"Uzinduzi huu wa Brazuka lazima ufikie malengo kwa sababu unaendeshwa na watu makini na Taasisi inayomiliki timu inayoshiriki ligi daraja la tatu iliyopo Songea, tumeangalia vijana wenye vipaji na hawaonekani kuwafuata huko na kuwapa nafasi ya kuonyesha uwezo wao na kuwaleta katika mikoa na baadaye kupata nafasi kwa timu za juu.

"Kama kweli tunataka kuendeleza soka letu la Tanzania lazima twende chini, Brazuka wamekuja na kampeni ya kuzunguka wilaya mbalimbali kwa ajili ya kutafuta vipaji," alisema Sebbo.

Aidha, alisema kampeni hiyo itawalenga vijana wenye umri chini ya miaka 20 na kuwapa nafasi ya kuonyesha kile walichonacho.

"Wachezaji ambao watapatikana hapa wataunda timu ya Brazuka FC ambayo itashiriki ligi daraja la tatu pamoja na kuwapeleka nje ya nchini, pia kazi kubwa tutakayoifanya ni kuchagua makipa kwa sababu sekta hiyo kwa sasa imekuwa na upungufu mkubwa," alisema Sebbo.

Kwa upande wake Mmiliki wa Brazuka, Mchata Erick, alisema jambo hilo ni kubwa kwa sababu watazunguka maeneo mengi zaidi.

Alisema wamefanya utafiti wa kutoshana kuona kuna changamoto ya vijana chini ya umri wa miaka 20 wenye vipaji kutoonekana kutokana na kuwa mbali na maeneo ya mijini.

"Brazuka tuko Songea na tunatumia uwanja wa Majimaji, tumeunda timu ya watu maalumu ya benchi la ufundi kwa ajili ya zoezi hilo na hao vijana watakaopatikana tutakuwa na zoezi la kuwatafutia timu iwe ndani au nje ya Tanzania," alisema Mchata.

Alisema baada ya kupata wachezaji hao kutakuwa na mechi za kirafiki kwa mikoa 10 ambayo tutaisaidia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuweza kupata wachezaji na kutengeneza timu yetu ya taifa ya vijana na baadaye ya wakubwa.

Aidha, Mkurugenzi wa ufundi wa Shirikisho la Soka TFF, Oscar Mirambo, alisema kampeni hiyo itaenda kuibua vipaji vingi na wao (TFF) watakuwa pamoja nao kuhakikisha jambo hilo linaenda kufanyika na kufanikiwa.



Kijana Ramadhan Rusambo (kushoto) na Saidy Kabengwa, wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Julio apania makubwa msimu ujao

**Na Abdallah Mataka**

BAADA ya kujihakikishia kubaki Ligi Kuu msimu ujao, Kocha wa KMC, Jamhuri Kiwhelo 'Julio' amesema anaiandaa timu yake kuja kuwa tishio msimu ujao na tayari ameanza kazi ya kukisuka upya kikosi hicho.

Akizungumza na Nipashe Julio alisema tayari timu hiyo imeanza maandalizi ya msimu mpya hivyo anaimani ripoti yake itafanyiwa kazi na viongozi katika kukiboresha kikosi hicho ili kiweze kufanya vizuri na kuondokana na hali waliyokutana nayo msimu huu ya kucheza mchezo wa mchujo 'Play off' kuwania kubaki Ligi Kuu.

"Wakati nakabidhiwa timu zilikuwa zimebaki mechi nne ligi kumalizika moja ya majukumu niliyopewa ni kuhakikisha timu haishuki daraja, nashukuru Mungu hili limetimia hivyo sasa maandalizi ya kupambania ubingwa wa ligi yameanza na sio kucheza tena 'play off' kama msimu huu," alisema Julio.

Aidha, Julio alisema anatambua ugumu uliopo kwenye ligi atatumia kipindi hiki cha usajili kuhakikisha anatengeneza timu bora itakayoleta ushindani na kufanya vizuri katika mashindano itakayoshiriki ikiwa pamoja na Ligi Kuu NBC pamoja na Kombe la Shirikisho la Azam.

Hata hivyo Julio alisema kwao KMC hakuna timu kubwa za kuzihofia kwenye Ligi bali kuna timu kongwe ambazo anatambua namna ya kuzikabili .

"Hakuna timu kubwa kwetu zaidi ni timu kongwe na hizi ninatambua mbinu zao sina mashaka nao tukikutana, kikubwa kwetu ni kupata pointi tatu ni suala la kusubiri, naandaa timu ya ushindani msimu ujao," alisema Julio .

Julio alisema anaamini kwa namna anavyoiandaa timu msimu ujao itakuwa moto wa kuotea mbali kwenye Ligi Kuu.

## Hatima Mbeya City, Mashujaa leo

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya Mbeya City kubaki Ligi Kuu au kushuka daraja, inajulikana leo Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya itakapoikaribisha Mashujaa FC katika mechi ya mkondo wa pili ya 'play off.'

Mbeya City itaingia uwanjani ikiwa na jeraha la kipigo cha mabao 3-1 ilichokipata Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, hivyo inahitaji ushindi wa mabao 2-0 na kuendelea ili ibaki Ligi Kuu, matokeo yoyote kinyume na hapo itakuwa imekata tiketi ya kushuka daraja.

Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Meja Mstaafu Abdul Mingange, amesema amepata meseji nyingi si kwa mashabiki wa Kigoma tu, hata maafande wa Jeshi la Wananchi Tanzania kuwa safari hii wanahitaji kuwa na timu kwenye Ligi Kuu kama ilivyo kwa majeshi mengine kama Polisi, Magereza na JKT.

"Mechi itakuwa ngumu, pamoja na kwamba mimi binafsi na wachezaji wangu tuna uhakika wa kushinda mechi hii, au kupata bao moja ambalo linaweza kutuweka sehemu nzuri ya kuhakikisha tunapanda, lakini mpira mara nyingi una maajabu yake na kuna vitu fulani niliviona kwenye mechi iliyopita si vizuri sana, tumeona mapungufu na nimeyafanyia kazi, tupo tayari kwa mchezo huu wa marudiano," alisema Mingange.

## Kidunda, Mfaume kupima afya leo

**Na Saada Akida**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Seleman Kidunda na Mfaume Mfaume wataongoza mabondia watakaocheza pambano la 'hata usipolala pata kucha' kufanya vipimo vya afya kabla ya pambano hilo linalotarajiwa kufanyika Juni 30, Mlimani City jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao wamesema wapo tayari kwa ajili ya mapambano hayo huku kila mmoja akijinasibu kufanya vizuri dhidi ya mpinzani wake.

Kidunda atapanda ulingoni siku hiyo kucheza na Erik Mukadi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Mfaume atapambana na Nkululeko Mhlongo siku hiyo katika mapambano yanayosubiriwa kwa shauku kubwa.

Akizungumza na Nipashe jana, promota wa pambano hilo kutoka kampuni ya 'PAF Promotion Limited' alisema kuwa wanatarajia kufanya vipimo vya afya kabla ya pambano hilo kwa lengo la kufikia kanuni na sheria za mchezo huo kwa mabondia watakaopanda ulingoni kwenye pambano hilo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FRED ATAKIWA BRAZIL
FULHAM inataka kumsajili kiungo wa Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 30, anayechezea klabu ya Manchester United. **(Telegraph)**

### JOHNSTONE ATAKIWA EVERTON
KLABU ya Everton ina nia ya kumnunua golikipa wa Crystal Palace na England, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 30, ikiwa Jordan Pickford ataondoka katika klabu hiyo. **(Sun)**

### MADDISON KUUZWA
LEICESTER City inataka zaidi ya pauni milioni 50 kumuuza kiungo wake, James Maddison mwenye umri wa miaka 26, huku Tottenham Hotspur na Newcastle United zikimwania. **(Sky Sports)**

### GVARDIOL SAFI MAN CITY
KLABU ya Manchester City inakaribia kufikia makubaliano binafsi na beki wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21. **(Fabrizio Romano)**

### OFA YA KAI
ARSENAL imetoa ofa iliyoboreshwa ya euro milioni 60 kwa mshambuliaji wa Chelsea na Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 24. **(Mail)**

### NEWCASTLE KUSITISHA
KLABU ya Newcastle United inafikiria kusitisha nia yake ya kumnunua kiungo wa kati wa Inter Milan na Italia, Nicolo Barella mwenye umri wa miaka 26. **(Independent)**

### HODGSON KUBAKIZWA
KLABU ya Crystal Palace inamtaka Roy Hodgson mwenye umri wa miaka 75 kubakia kama kocha wao. **(Guardian)**


### VALVERDE AWANIWA
KLABU za Manchester City, Chelsea na Liverpool zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Real Madrid na Uruguay, Fede Valverde mwenye umri wa miaka 24 msimu huu. **(Teamtalk)**

### PEREZ MKATABA WA KUDUMU
KLABU ya Real Betis inataka kuafikiana mkataba wa kudumu na fowadi wa Hispania, Ayoze Perez mwenye umri wa miaka 29 ambaye alijiunga kwa mkopo kutoka Leicester Januari. **(AS)**

### KIMMICH HAUZWI
KLABU ya Bayern Munich imesema haina nia ya kumuuza Joshua Kimmich na imeikosoa Barcelona kwa 'kufanya mzaha' ili kumvutia kiungo huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28**. (Sky Sport Germany, via Goal**)

### HAZARD KUCHEZA NYUMBANI
BAADA ya kukatisha mkataba wake na Real Madrid, fowadi wa zamani wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 32 anafikiria kurejea nyumbani kucheza pamoja na mdogo wake Kylian katika klabu ya RWD Molenbeek.**(Sacha Tavolieri)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AWEKA REKODI MECHI 200 KIMATAIFA

Amekuwa mwanasoka wa kwanza kwa wanaume kucheza mechi 200 za kimataifa wakati...

**REYKJAVIK, Iceland**

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mwanasoka wa kwanza kwa wanaume kucheza mechi 200 za kimataifa wakati wa ushindi wa Ureno wa kufuzu michuano ya euro 2024 dhidi ya Iceland siku ya Jumanne.

Nahodha huyo wa Ureno, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa mwaka wa 2003, alifikia hatua hiyo muhimu katika mji Reykjavik kwenye uwanja wa Laugardalsvollur na kufunga bao la ushindi katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Iceland.

"Nina furaha sana. Kufikisha mechi 200 ni aina ya wakati ambao hutarajii kamwe. Ni mafanikio ya kushangaza. Na bila shaka kufunga bao la ushindi kunaifanya kuwa siku ya kipekee zaidi," alisema Ronaldo baada ya mchezo huo.

Ronaldo alilazimika kusubiri dakika mbili ili kushangilia bao hilo la ushindi kwani awali mwamuzi alikataa kwa madai ya kuwa ameotea, lakini marudio ya VAR yakamzawadia.

Lilikuwa bao la 123 kwa Ronaldo kwa Ureno, na kuendeleza rekodi yake ya kuwa mfungaji bora wa muda wote wa kimataifa.

Mshambulizi huyo wa Al-Nassr tayari alishikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi za kimataifa alipoipita ile ya Bader Al-Mutawa wa Kuwait, ambaye alishikilia rekodi ya mechi 196. Kabla ya mechi dhidi ya Iceland, Ronaldo alipokea tuzo ya rekodi ya Dunia ya Guinness kuadhimisha kuwa mchezaji wa kwanza wa kiume kucheza katika mechi 200 za kimataifa.

Matokeo hayo yameiacha Ureno kileleni kwa pointi 12, mbili mbele ya Slovakia iliyo nafasi ya pili, ambayo ilishinda 1-0 ugenini dhidi ya Liechtenstein mapema Jumanne.

Ronaldo aliongeza: "Michezo 200 iliyochezwa inathibitisha mapenzi niliyonayo kwa nchi yangu. Kwangu mimi ni hatua muhimu sana. Ina maana kubwa. (200) ni namba nzuri ambayo (hakuna mchezaji wa kiume) anayo. Ninajivunia sana kwa sababu hili ni jambo ambalo sikuwahi kufikiria ningeweza kufikia. Na ninaendelea kuweka rekodi."

Katika Kombe la Dunia la 2022 huko Qatar, Ronaldo alikuwa mchezaji wa kwanza wa kiume kufunga katika fainali tano tofauti za Dunia.

Mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, Ronaldo ana heshima mbili kuu akiwa na Ureno -- aliiongoza nchi yake kutwaa Euro 2016 na kombe la Ligi ya Mataifa ya Uefa miaka mitatu baadaye.

HABARI MICHEZO



# N'GOLO KANTE RASMI MALI YA AL ITTIHAD

**RIYADH, Saudi Arabia**

MSHINDI wa Kombe la Dunia na Ufaransa, N'Golo Kante, amekubali kujiunga rasmi na mabingwa wa Ligi Kuu ya Saudi Araba, Saudi Pro League, Al Ittihad kwa mkataba wa miaka mitatu mara muda wake Chelsea utakapokamilika mwishoni mwa mwezi huu, klabu hiyo imetangaza.

Kante, ambaye mkataba wake na Chelsea unamalizika rasmi Juni 30, ataungana na Karim Benzema katika klabu hiyo yenye maskani yake Jeddah na linakuwa jina lingine kubwa la hivi karibuni kuhamia Saudi Arabia kufuatia uhamisho wa Cristiano Ronaldo kwenda Al Nassr mwezi Januari.

"Kante alisaini mkataba Jumanne, Juni 20, baada ya kukamilisha vipimo vyake vya afya katika kituo maalumu cha matibabu huko Dubai," ilisema taarifa ya Al-Ittihad.

"Hatua hii inakuja wakati Ittihad, ambayo hivi majuzi alishinda Ligi Kuu ya Saudia, analenga kuimarisha kikosi chake.

"Kuongezwa kwa Kante Al-Ittihad kunachukuliwa kuwa moja ya usajili wa hali ya juu na wenye matokeo katika historia ya klabu. Ni sehemu ya juhudi za klabu kujiweka kama chaguo bora kwa wachezaji wa kiwango cha kimataifa katika Ligi ya Saudia."

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 utamfanya kulipwa euro milioni 86 kwa mwaka.

ESPN iliripoti Februari kwamba Kante alikuwa karibu kusaini mkataba mpya na Chelsea, lakini hakuna dili lililokamilishwa na kiungo huyo sasa ameamua kumaliza miaka saba ya kukaa pale Stamford Bridge.

Baada ya kucheza jukumu muhimu katika ushindi wa kushangaza wa Leicester City wa Ligi Kuu mwaka 2016, Kante alihamia London Magharibi, ambapo alikuwa mchezaji wa kwanza tangu Eric Cantona mwaka 1993 kushinda mataji mfululizo ya Ligi Kuu akiwa na timu mbili tofauti.

Mafanikio zaidi yalifuata wakati wa kubeba Kombe la FA mwaka wa 2018 na kushinda Ligi ya Europa mwaka uliofuata kabla ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka wa 2021. Lakini majeraha yalimfanya acheze mara tisa pekee katika michuano yote msimu uliopita wakati Chelsea ikiwa kwenye msukosuko.

Licha ya kutumia zaidi ya pauni milioni 600 kununua wachezaji wapya tangu Todd Boehly na Clearlake Capital wachukue klabu hiyo Mei mwaka jana, Chelsea walimaliza wakiwa nafasi ya 12 katika Ligi Kuu.

Thomas Tuchel na mbadala wake Graham Potter wote walifutwa kazi kama makocha wakati wa kampeni kabla ya msimu kumalizika huku Frank Lampard akichukua nafasi ya uongozi wa muda.

Baada ya kuteuliwa kwa Mauricio Pochettino kama kocha mpya mwezi uliopita, inatazamiwa kuwa majira mengine ya joto ya Chelsea huku wachezaji kadhaa -- wakiwamo Christian Pulisic, Mateo Kovacic na Mason Mount wakitarajiwa kuondoka.

# Mkataba mpya wamsubiria Rashford

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ina uhakika kuwa inakaribia kukubaliana kuhusu mkataba mpya na wa muda mrefu na mshambuliaji wake, Marcus Rashford, vyanzo vimeiambia ESPN.

Rashford atangia mwaka wa mwisho wa mkataba wake msimu huu wa joto lakini, baada ya mazungumzo kuongezwa kuelekea mwisho wa msimu uliopita, mshambuliaji huyo wa England anaelekea kuongeza muda wake wa kukaa Old Trafford.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Rashford anatazamiwa kupewa mkataba mpya ambao utamfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alicheza vyema katika msimu wake wa kwanza chini ya Erik ten Hag, akifunga mabao 30 katika mashindano yote na 17 katika Ligi Kuu ya England.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba maendeleo yaliyopatikana chini ya Ten Hag yamekuwa sababu kuu katika uamuzi wa Rashford kubakia.

Paris Saint-Germain wameonesha nia siku za nyuma wakati wa Manchester City, Pep Guardiola na yule wa Chelsea, Mauricio Pochettino



wote wanavutiwa nae, lakini Rashford mwenyewe alikuwa na nia ya kubaki Man United.

Ten Hag anatarajia kurekebisha safu yake ya ushambuliaji wakati wa usajili wa majira ya joto na kuongeza mshambuliaji mwingine.

Kuna nia ya Harry Kane, Victor Osimhen, Rasmus Hojlund, Randal Kolo Muani na Lautaro Martinez, lakini hadi sasa United wametatizwa na vikwazo vyao vya bajeti na kile wanachoamini kuwa tathmini zisizo za kweli.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba klabu hiyo ina kati ya pauni milioni 100 na pauni milioni 150 za kutumia kununua wachezaji wapya msimu huu wa joto, ingawa idadi hiyo itaimarishwa na fedha zitakazopatikana kutokana na wanaoondoka.

United wako tayari kusikiliza ofa kwa wachezaji kadhaa wa kikosi cha kwanza wakiwamo Harry Maguire, Fred, Anthony Martial, Scott McTominay, Donny van de Beek, Anthony Elanga, Eric Bailly, Alex Telles, Brandon Williams na Dean Henderson.

# Son Heung-Min akataa kuhamia Saudia Arabia

**LONDON, England**

NYOTA wa Tottenham Hotpur, Son Heung-Min, ametangaza nia yake ya kubakia klabuni hapo licha ya kupokea ofa nono ya kujiunga na klabu ya Saudi Arabia, Al Ittihad.

ESPN ilifichua Jumatatu kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amekuwa akilengwa na Klabu za Saudia huku Al Ittihad ikimpa fowadi huyo ofa ya mkataba wa miaka minne wenye thamani ya euro milioni 30 kwa msimu.


Chanzo kilicho karibu na mazungumzo kilidokeza kuwa upande wa Saudia ulikuwa unaandaa dau la ufunguzi la euro milioni 60 pamoja na bonasi, lakini Tottenham walisema hawakutaka kusikiliza ofa za fowadi huyo raia wa Korea Kusini.

Akizungumza Jumanne, Son aliamua kuzima uvumi juu ya uhamisho kwa kusisitiza kujitolea kwake kwa Spurs.

Son amenukuliwa na ripota wa soka wa Korea, Sungmo Lee akisema: "Nina mambo mengi ya kufanya katika Ligi Kuu. Fedha haijalishi kwangu sasa, na fahari ya kucheza soka, kucheza ligi ninayoipenda ni muhimu, nataka kuichezea Tottenham zaidi kwenye Ligi Kuu. Nitajiandaa vyema nitakaporejea Spurs."

Chanzo hicho kilidokeza kuwa kulikuwa na matumaini kwamba Son anaweza kujaribiwa kuhamia Al Ittihad kutokana na klabu hiyo kuwa tayari imekubali dili la kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema, huku kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante akiwa tayari ametambulishwa juzi.

Mkataba wa sasa wa Son na Tottenham unamalizika mwaka 2025.



# SERIKALI YATAKA WAZAWA KUMILIKI KAMPUNI ZA KUBET

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imependekeza kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania kuweka takwa la kisheria la kutoa leseni za michezo ya kubahatisha kwa kampuni ambayo angalau asilimia 25 ya hisa zake zinamilikiwa na Watanzania.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha bungeni juzi muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 unaolenga kurekebisha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali ili kuleta maana sahihi iliyokusudiwa katika masharti ya sheria.

Alisema katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 13 serikali inapendekeza marekebisho hayo kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Watanzania kuwekeza katika biashara ya michezo ya kubahatisha.

Aidha, alisema kifungu cha 26 cha sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu kuanzishwa kwa michezo ya meza isiyozidi miwili katika maeneo yenye mashine za sloti arobaini kwa mujibu wa kanuni ili kuongeza wigo wa kodi.

"Vilevile, marekebisho yanafanyika katika Jedwali la Pili la Sheria kwa kupunguza kiwango cha kodi kutoka asilimia 25 hadi asilimia 18 kwenye mapato ghafi ya michezo ya kubahatisha kwenye mashine arobaini za sloti na lengo ni kuleta usawa katika utozaji wa kodi kwenye michezo ya kubahatisha inayoshabihiana,"alisema.



Watoto wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yakiri 'fukuza fukuza' makocha iliwanyima ubingwa

INATOKA UK. 24

kwenye kiwango kizuri, msimu uliofuata kuna wachezaji waliondoka Simba na tusingeweza kuwabakisha kutokana na fedha zilizokuwa zimewekwa kwa ajili ya kuwachukua pia kuna kocha aliondoka muda mfupi baada ya kutufikisha robo fainali, yote kwa sababu ya pesa, ilitudhoofisha pia," aliongeza kusema Mangungu na kuongeza,

"Hatuna uchumi mkubwa hivyo tunazidiwa na walio na uchumi mkubwa kwa kuwachukua wachezaji wazuri na wenye vipaji na makocha wazuri kwa sababu ukiangalia makocha waliopita Simba sasa hivi wako wapi, hivi karibuni tumeona makocha wetu wakipata timu kubwa akiwemo Sven," aliongeza Mangungu.

Alisema kwa sasa wanajipanga vizuri kwa msimu ujao kwenye mashindano ya Kimataifa na ya kitaifa ambapo moja ya jambo waliloliamua ni kumpa muda mrefu kocha wao, Robertinho ili wafikie malengo yao.

"Tunataka kufanya vizuri msimu ujao, Uongozi tunajipanga kufikia malengo yetu, tunataka kurejesha mataji yetu lakini pia kuvuka hapa tunapoishia kwenye mashindano ya kimataifa, tumeweka mikakati yetu vizuri na mashabiki wasubiri kuona tutakachokifanya," alisema Mangungu.

Simba msimu uliopita waliishia hatua ya robo fainali ya klabu bingwa Afrika lakini pia kwa msimu wa pili mfululizo wameshindwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania bara na hata Kombe la Shirikisho la Azam.

## Ajibu aimarika kwa msimu ujao

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa Singida Fountain Gate FC, Ibrahim Ajibu, ameendelea kuimarika kutokana na majeraha aliyokuwa nayo hali iliyompelekea kukaa nje kipindi cha miezi mitatu.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Ajibu alisema kwa sasa anaendelea vyema na tayari ameanza kufanya mazoezi mepesi.

"Ninashukuru hali yangu inaendelea vizuri baada ya kukaa nje muda mrefu ninaamini msimu ujao nitakuwa nimeimarika zaidi, alisema Ajibu.

Alisema maendeleo yake ya sasa yanampa matumaini ya kuanza mazoezi mapema ya kujiweka sawa kuelekea kwenye msimu ujao ambao ameahidi kufanya vizuri zaidi.

Mshambuliaji huyo alisema alishindwa kuonyesha makali yake msimu uliopita kufuatia majeraha hayo na kuahidi kuendeleza kiwango chake.

"Nitarudi tu kwenye kiwango changu, kikubwa ilikuwa kupona kwanza, nashukuru Mungu hali yangu ya sasa, nimeanza mazoezi mepesi na ndani ya muda mfupi nitarejea kwenye mazoezi ya nguvu kabla ya kuanza maandalizi na timu yangu kuelekea kwenye msimu mpya," alisema Ajibu.

Ajibu alijiunga na Singida Big Stars (Sasa Singida Fountain Gate) msimu uliopita akitokea Azam FC ambapo hakupata nafasi kubwa ya kucheza.

## Msuva aipa Yanga nafasi kumsajili, Ambundo apewa 'Thank you'

INATOKA UK. 24

kizuri tu," alisema.

Msuva aliichezea Azam FC 2010, na 2011 alijiunga na Moro United kabla ya kuchukuliwa na Yanga 2012 ambapo aliichezea hadi 2017 alipotimukia Morocco kujiunga na Difaa El Jadida.

Mwaka 2020 alijiunga na Wydad Athletic Club ya Casablanca nchini humo hadi mwaka jana alipojiunga na Al-Qadsiah ya Saudi Arabia ambayo tayari amemaliza mkataba wake.

Wakati huo huo, Yanga imetangaza kuachana na winga wake Ambundo iliyomsajili misimu miwili iliyopita kutoka Dodoma Jiji.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo wamefikia makubaliano ya kuachana naye na kumtakia kila la heri atakapoenda.

Michezo
Alhamisi Juni 22, 2023
Nipashe



Ronaldo aweka rekodi mechi 200 kimataifa UKURASA 21


Murtaza Mangungu

# SIMBA YAKIRI 'FUKUZA FUKUZA' MAKOCHA ILIWANYIMA UBINGWA

## ●●●Yasema uchumi mdogo pia sababu ya kupoteza wachezaji, makocha wazuri, msimu huu yapanga...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umeweka wazi kuwa kubadilisha makocha mara kwa mara kuliwagharimu na kujikuta wakifanya vibaya misimu miwili mfululizo kwenye mashindano ya ndani na ile ya kimataifa.

Aidha, imesema uchumi mdogo wa Tanzania ni sababu nyingine zilizozigharimu timu za ndani kuwania wachezaji wazuri wa kimataifa au kuwabakisha wachezaji wa kimataifa waliofanya vizuri.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu alisema kutokana na makosa hayo msimu huu wameyafanyia kazi ambapo wameamua kubaki na kocha wao Robert Oliviera 'Robertinho' na kumpa muda wa kuitumikia timu hiyo.

"Ukiangalia katika misimu mitatu Simba imefundishwa na makocha sita kitu ambacho kimechangia kuanza upya kila msimu, haya ni makosa tuliyoyafanya na hatutaki kuyarudia tena, katika kipindi hiki ninachokizungumzia baadhi ya makocha waliotufundisha ni Didier Gomes, Pablo Franco, Sven Vanderbroeck na Zaron Maki ambao walipita na kuondoka," alisema Mangungu.

"Lakini hatuwezi kusita kusema hali ya kiuchumi nayo imekuwa ikichangia timu zetu kutokuwa na mtiririko ule ule wa wachezaji, tunakuwa na wachezaji wazuri lakini wakishaonekana tu nje ya nchi inakuwa ngumu kuwabakisha kutokana na uwezo wa kiuchumi kwa hizo timu zinazowahitaji," alisema Mangungu.

"Kama mnakumbuka wakati tukiwa

INAENDELEA UK. 23

# Msuva aipa Yanga nafasi kumsajili, Ambundo apewa 'Thank you'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI winga wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Simon Msuva akiipa nafasi timu yake ya zamani Yanga kumsajili pale atakapoona inatosha kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, klabu hiyo imeachana na winga wake Dickson Ambundo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Msuva amesema tayari amemaliza mkataba wa timu aliyokuwa anaichezea Al-Qadsiah ya Saudi Arabia, hivyo anakaribisha ofa mbalimbali kwa klabu ambazo zinamhitaji.

Amesema bado akili yake inawaza kucheza soka nchi za nje kwa ajili ya kutengeneza maisha yake, pamoja na msaada kwenye kikosi cha timu ya taifa, Taifa Stars.

"Bado akili yangu inafikiria kucheza nje ya nchi, kwa sasa sina sababu ya kurejea nchini, umri bado unaruhusu na nina nguvu za kutosha kwa mwili wangu huu siwezi kuzeeka leo, lakini kama nitarudi nyumbani timu ninayoipa nafasi ni Yanga kwa sababu ndiyo timu niliyotoka na kila mtu anajua hilo kama nikirudi nyumbani timu yangu ya kuichezea ndiyo hiyo, japo pia inaweza ikawa Azam, wengi hawajui kuwa nimeshawahi kuichezea, mimi timu kubwa ambayo sijaichezea hapa ni Simba tu," alisema.

Alisema aliondoka kwenye kikosi cha Yanga akiwa tegemeo, lakini anashukuru wanachama, mashabiki na viongozi wa Yanga walimruhusu kwa roho moja na kumfanya afanye vizuri alikokwenda.

"Niliondoka Yanga na ilikuwa si rahisi kwa kipindi kile kuniruhusu hasa ikizingatiwa nilikuwa nimetoka kuwa mfungaji bora na mchezaji bora nilicheza misimu miwili kwa kiwango cha juu, lakini wanachama, mashabiki na viongozi wakaniruhusu, wakaniombea dua na kweli hata nilipoondoka kwenda Morocco hadi leo nimekuwa kwenye kiwango

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >